epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

epaper.ippmedia.com | 0745 700710
www.ippmedia.com | LIKE & FOLLOW US
Jumatatu Januari 20, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581927
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

# Imeisha hiyo

• **CCM** yawapitisha Samia, Mwinyi kuwania urais 2025, miradi ya kimkakati yawabeba... *Endelea ukurasa 2 & 3*




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan (kulia), akijadiliana jambo na Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa siku ya pili ya Mkutano Mkuu Maalumu wa Chama hicho, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 7
**Utapeli** mamilioni unavyowaliza watu Mlimani City

UKURASA WA 17
**Zanzibar** yatangaza bei mpya za umeme



UKURASA WA 19
**Trump** kuapishwa leo, maandamano yaitishwa Marekani



UKURASA WA 12
**FOWADI 6 WANAOWEZA KUMRITHI JESUS ARSENAL**

RIPOTI MAALUMU
## Taka hatari za hospitalini zatapakaa ufukweni
UKURASA 4



## Mbowe aahidi matano, Lissu azidi kuwavutia wenyeviti
UKURASA 5



**MICHEZO** **RAMOVIC: USHINDI KIRAHISI UMETUPONZA CAF** UK.24

**KATUNI** UK.6



Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete akitoa ushauri kwenye mkutano Mkuu maalumu wa chama hicho, jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# CCM yawapitisha Samia na Mwinyi kuwania urais 2025

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIJANA wa mitaani wana kauli yao "imeisha hiyo" wakiwa na maana ya kuwa na uhakika wa kutimia kwa jambo lao. Wajumbe wa vikao vya juu ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) nao wameshakamilisha mapema.

Hii ni baada ya ya Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM kupitisha azimio kuwa Rais Samia Suluhu Hassan wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wa Zanzibar kuwa wagombea wa nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Wajumbe wa mkutano huo walifikia hatua hiyo jana baada ya kusomewa taarifa ya utekelezaji Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 ambayo ilionesha chini ya uongozi wao wametekeleza miradi ya maendeleo na ya kimkakati vizuri na inawagusa wananchi.

Akisoma azimio hilo, Mjumbe na Mbunge wa Viti Maalumu, Ng'wasi Kamani, alisema kwa kuzingatia mamlaka waliyonayo wajumbe chini ya Ibara ya 101(5)(b) ya Katiba ya CCM, wanaazimia jina la Samia kuwa ndiye mwanachama atakayesimama kugombea kwenye Uchaguzi Mkuu 2025 kwa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, alisema chini ya Ibara ya 103(c) ya Katiba hiyo, Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) ndio yenye mamlaka ya kuchagua jina moja la wanachama atakayesimama kugombea urais wa Zanzibar na jana walielekeza NEC kukutana kutekeleza jukumu hilo la kumchagua Mwinyi kuwa mgombea wa urais Zanzibar.

Kabla ya kufikiwa hatua hiyo, kutokana na hoja za wajumbe, Rais Samia alisema anaogopa kuzungumza na kuomba ushauri kwa viongozi wastaafu kama jambo hilo linawezekana.

Akifafanua kuhusu hilo, Mwenyekiti mstaafu wa CCM na Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, alisema kila chama kina utaratibu wake wa kuteua wagombea na uamuzi ni wa kikao hicho na kwamba kuna nchi kama Namibia wanafanya uamuzi wa wagombea mwaka mzima.

"Kama tunataka kuamua leo (jana) Samia na Mwinyi ni wagombea wetu, mamlaka hayo tunayo. Kama tunaamua hivyo ndio tumeamua, kilichobaki ni ushauri wa wale wanaojua taratibu za sheria, lakini watu wote watajua tu kuwa CCM kwenye uteuzi wa wagombea imemaliza," alisema.

Alisema kazi kubwa imefanywa na viongozi hao kupitia taarifa ya utekelezaji ilani iliyowasilishwa kwenye mkutano huo, imeonesha wana-CCM hawakukosea kwa kuwa ni watu makini, wanajua wanachofanya na kinachotakiwa kufanyika.

"Ushindi wa CCM ni dhahiri, ushindi kwa mwaka huu hauna mjadala, wagombea watakuwapo wa vyama vingine lakini sioni namna wanavyoweza kuishinda CCM, lakini si kwa ujanjaujanja, yapo mambo mengi mazuri yaliyofanywa na serikali zetu na yana manufaa kwa watanzania.

"Mnaweza kufanya mambo mengi mazuri lakini hayajawagusa wananchi. Haya yanagusa maisha," Kikwete alisema.

Aliongeza kuwa wananchi watatambua na kuthamini kazi iliyofanywa na viongozi hao na kushauri wana-CCM wasibweteke.

"Siku zote jipe rai kwamba uchaguzi huu utakuwa mgumu. Hiyo ndio falsafa ya jeshi, maandalizi yetu yawe kwamba tunakwenda kwenye vita kubwa na si ndogo na tujiandae kwamba tunakwenda kwenye mapambano makubwa.

"Lazima tujiandae vizuri, na mimi niliyoyasikia hapa, bwana aah! Sijui labda kutokee mchawi na wachawi walishakufa, hapo tena," alisema.

Kikwete alisema wajumbe wa mkutano wanamtaka Samia na Mwinyi waendelee na kwamba hakuna wa kusema 'hapana'.

"Namna ya kulifanya jambo hili, liandaliwe azimio maalumu la mkutano ili kutamka, liletwe na ithibitishwe na linakubaliwa na inakuwa sasa rasmi uamuzi wa mkutano mkuu," alisema.

Mwenyekiti mstaafu huyo pia aliwaomba viongozi na wajumbe kuwaeleza wanachama na wananchi yaliyofanyika chini ya uongozi wa Rais Samia na Mwinyi na sababu ya kuwapitisha kuwapa ridhaa tena.

Vilevile, alimpongeza Katibu Mkuu Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa utendaji wake mzuri huku akieleza kuwa Makamu Mwenyekiti mpya, Stephen Wasira anajulikana kwa uwezo wake wa uongozi, kupambana na kujenga hoja, hivyo nafasi hiyo imepata mtu madhubuti.

Alisema mkutano huo umemwonesha sura ya CCM anayoijua kwa kuwa mikutano mikuu ndio inaonesha nguvu ya kuendelea mbele na hana shaka wajumbe watarudi na nguvu mpya.

Baada ya ufafanuzi huo, Mwenyekiti Samia alielekeza Sekretarieti ya CCM Taifa ikaandae azimio hilo na kupeleka kwenye mkutano huo.

Awali, miongoni mwa wajumbe waliozungumzia suala hilo ni Mbunge wa Mvumi na Mjumbe wa Mkutano Mkuu, Livingstone Lusinde, aliyesema ilani imetekelezwa kwa zaidi ya asilimia 100 na kwamba hakuna deni, wananchi wameona yaliyofanyika kwenye sekta za afya, elimu na miundombinu.

Alisema mkutano huo ni mkubwa na wenye uamuzi, hivyo akaomba wajumbe wafanye uamuzi ili mwenyekiti aone uzito wa mkutano huo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma, Adam Kimbisa alisema wajumbe wameshuhudia miradi iliyotekelezwa na hakuna ambaye hajaguswa na kuomba wajumbe waazimie kuwapitisha Samia na Mwinyi wawe wagombea wa nafasi ya urais.

Kwa kupitishwa huko, Samia atakuwa mgombea urais wa kwanza mwanamke kupitia CCM tangu Uchaguzi Mkuu wa kwanza nchini mwaka 1995.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# TRA yajivunia kupaa makusanyo

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mcha Hassan amesema Mkoa wa kikodi Kariakoo katika nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/25 umekusanya Sh. bilioni 71 .7 kwa kipindi cha miezi sita ya kwanza sawa na ufanisi wa asilimia 104.

Mcha alisema hayo jana wakati wa bonanza la kuelekea kilele cha mlipakodi Januari 23 mwaka huu, lililoandaliwa na TRA Mkoa wa Kikodi Kariakoo kwenye viwanja vya Jakaya.

Alisema Kariakoo ni mkoa wa kikodi wa kimkakati na kwamba umefanikiwa kukusanya kiwango hicho kutokana na kusogeza huduma muhimu kwa wafanyabiashara 30,000 wanaotegemea soko hilo.

"Kama tunavyojua, soko hili linategemewa na watu kutoka Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na Visiwa vya Comoro," alisema.

Mcha alisema kwa mwaka huu Kariakoo itaendelea kuwa kiungo muhimu pamoja na kushirikisha wadau mbalimbali kwenye matukio ya pamoja ili kukuza na kuimarisha uhusiano uliopo kati ya sekta binafsi na mamlaka hiyo.

Aliwashukuru wafanyabiashara wa Kariakoo kwa kuendelea kulipa kodi kwa hiari kukuza Pato la Taifa na kuwaahidi kuendelea kufanya nao kazi kwa weledi na ubunifu kupitia mikakati yote waliyoweka.

Alisema wataendelea kuongeza idadi ya wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi, kuongeza huduma mashine za kielektroniki kwenye sekta hiyo.

"Tumekuwa tukiweka mikakati mingi ambayo mingine inalenga kuwasaidia wafanyabiashara wote na hawa si wa ndani tu, hata wengine wanaotoka nje ya nchi, na tutaendelea pia kusisitiza watu walipe kodi kwa hiari ili kuepuka changamoto ndogondogo," alisema Mcha.

Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Kariakoo, Severin Mushi alisema kuwa kwa sasa wafanyabiashara wako tayari kulipa kodi kwa hiari na hayo ni matunda ya mikutano iliyofanyika kati yao na TRA.

HABARI KITAIFA

UTEKELEZAJI ILANI YA CCM

# Maboresho bandari, SGR yaleta mageuzi kiuchumi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar zimeanika namna zilivyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025, huku maboresho ya bandari na safari za treni ya mwendokasi (SGR) yakitajwa kuleta mageuzi ya kiuchumi.

Katika taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha Novemba 2020 hadi Desemba 2024 iliyowasilishwa kwenye Mkutano Mkuu maalumu wa CCM jana na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ilielezwa kuwa tangu kuzinduliwa safari za treni ya SGR Dodoma hadi Dar es Salaam Agosti 2024 hadi Desemba 11, 2024, zaidi ya abiria 1,200,000 wamesafiri na kuingiza mapato ya Sh. bilioni 30.

Akizungumzia kuhusu maboresho ya uendeshaji huduma za Bandari ya Dar es Salaam, Majaliwa alisema kuwa Mei 2024 hadi Novemba 2024, serikali imekusanya Sh. bilioni 62.44 kama tozo ya pango na mrabaha.

Alisema makusanyo hayo hayajumuishi tozo za huduma nyingine ambazo zinaendelea kutolewa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), ikiwamo huduma kwa meli na tozo ya matumizi ya miundombinu ambazo kwa pamoja ni Sh. bilioni 451.39 kwa kipindi hicho.

Majaliwa alisema kuwa mafanikio hayo yamechagizwa na uwekezaji uliofanywa katika mitambo ya kisasa na kutumia mifumo iliyoboreshwa ya TEHAMA kuhudumia shehena ya makasha.

Alisema tani milioni 5.022 ambayo ni zaidi kwa asilimia 15 ya shehena zimehudumiwa kulinganishwa na tani milioni 4.375 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita.

"Idadi ya makasha iliyohudumiwa na DP World katika kipindi cha Mei, 2024 hadi Novemba, 2024 ilifikia makasha ya futi ishirini (TEUs) 139,719 sawa na ongezeko la asilimia 44 ya makasha (TEUs) 96,854 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita," alisema.

Majaliwa alisema kuwa wastani wa muda wa meli kusubiri kushusha mzigo umepungua hadi kufikia siku saba kwa kipindi cha Mei, 2024 hadi Novemba, 2024 kulinganishwa na wastani wa siku 46 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita (Mei, 2023 hadi Novemba 2023).

Alisema kwa upande wa meli za makasha, hadi kufikia Oktoba 2024, DP World imefanikiwa kuondoa kabisa muda wa meli kusubiri kuingia bandarini na pindi zinapowasili katika Bandari ya Dar es Salaam huendа moja kwa moja gatini.

Alisema gharama za matumizi kwa Bandari ya Dar es Salaam zimepungua kwa wastani wa asilimia 47.

Alifafanua kuwa awali matumizi yalikuwa wastani wa Sh. bilioni 34.52 kwa mwezi katika kipindi cha Mei, 2023 hadi Novemba, 2023 ambayo yamepungua hadi wastani wa Sh. bilioni 17.93 kwa mwezi katika kipindi cha Mei, 2024 hadi Novemba 2024.

**MAJI, ELIMU**

Majaliwa alisema miradi 1,633 ya maji imetekelezwa, ikiwamo 1,335 ya vijijini na 298 ya mijini na kuongeza upatikanaji maji vijijini kutoka asilimia 70.1 hadi asilimia 79.6 na mijini kutoka asilimia 84 hadi asilimia 90.

Waziri Mkuu alisema bajeti ya elimu bila ada imeongezeka kutoka Sh. bilioni 312.5 mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 796.38 mwaka 2024 na wanafunzi wanaonufaika wameongezeka kutoka 14,940,925 mwaka 2020 hadi 16,155,281 mwaka 2024.

Alisema miundombinu ya shule za msingi na sekondari pia imeboreshwa na idadi ya shule za msingi imeongezeka kutoka 16,656 mwaka 2020 hadi 19,783 mwaka 2024.

Vilevile, alisema shule 26 za sekondari za wasichana za kidato cha tano na sita zimejengwa katika mikoa 26, ili kuhakikisha wanafunzi wa kike wanapata elimu bora.

**AFYA, UTALII**

Majaliwa alisema sekta ya afya imeimarishwa kupitia ujenzi wa vituo vipya na kuboresha huduma, huku miundombinu na upatikanaji vifaa tiba, vikipewa kipaumbele.

Alisema vituo vipya vya kutolea huduma za afya 183 vimejengwa, vikiwamo vyenye uwezo wa huduma za dharura za uzazi. Idadi ya vitanda vya hospitali imeongezeka hadi 126,209, ikiwa ni uwiano wa vitanda 2.1 kwa kila watu 1,000 karibu sawa na viwango vya Shirika la Afya Duniani.

Majaliwa alisema idadi ya watalii imeongezeka kutoka 620,867 mwaka 2020 hadi watalii 1,924,240 Novemba, 2024. Vilevile, mapato yatokanayo na shughuli za utalii yameongezeka kutoka dola za Marekani milioni 700 mwaka 2020 hadi dola za Marekani bilioni 3.3 mwaka 2024.

Akizungumzia utekelezaji ilani hiyo kwa upande wa Zanzibar, Makamu wa Pili wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema maelekezo sita yaliyotolewa na CCM kwa Serikali ya Zanzibar yametekelezwa.

Alisema shule 114 za msingi na sekondari zimejengwa mijini na vijijini na kwamba kiwango cha ufaulu kimeongezeka kutoka asilimia 55.4 kwa mwaka 2020 hadi asilimia 85.6 kwa mwaka 2023 kwa wanafunzi wa kidato cha nne huku cha sita ufaulu ukifikia asilimia 99.9.

Makamu wa Rais alibainisha kuwa katika sekta ya afya, ujenzi wa hospitali 10 za wilaya umekamilika na huduma za kibingwa zinapatikana Unguja na Pemba.

Alisema upatikanaji maji umefikia asilimia 88.22, visima 102 vimechimbwa, vijiji 222 vimefikiwa na umeme sawa na zaidi ya asilimia 72.

Pia alisema mchango wa utalii kwenye pato la taifa umefikia asilimia 30 na idadi ya watalii imeongezeka na kufikia 736,755 sawa na asilimia 183 kwa mwaka 2024 na mafanikio yamefikiwa kutokana na filamu ya 'Royal Tour', huku miradi ya utalii ikifikia 1,695.

Makamu wa Rais alisema masoko makubwa yamejengwa na vituo zaidi ya 14 vya wajasiriamali, kiwanda cha kuchakata mwani tani 30,000 kimejengwa na kitakuwa ni kikubwa kwa Afrika, kikitarajiwa kuzalisha ajira 25,000 rasmi na zisizo rasmi 66,000.

Pia alisema visiwa 21 vimetangazwa kwa ajili ya uwekezaji na tayari 15 vimepata wawekezaji, miradi 424 imeanzisha ajira rasmi zaidi 22,382 na zisizo rasmi zaidi ya 100,000.

Alisema pensheni jamii kwa wazee waliofikisha miaka 70 wanalipwa Sh. 50,000 kila mwezi na kwa wastaafu imefikia Sh. 180,000.




Sehemu ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa CCM Taifa, wakiwa kwenye Mkutano huo, jana. **PICHA: IKULU**

RIPOTI MAALUM

# Taka hatari za hospitalini zatapakaa ufukweni

## -Wananchi, viumbe-bahari hatarini...

Na Jenifer Gilla

WATUMIAJI fukwe zilizo karibu na mito inayomwaga maji Bahari ya Hindi katika Manispaa ya Kinondoni, mkoa wa Dar es Salaam, wako hatarini kukumbwa na maradhi kama vile saratani, tetenasi na kuambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU), imebainika.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa habari hii, umebaini baadhi ya fukwe katika manispaa hiyo zina taka hatarishi za hospitalini zinazomwagwa katika mito inayomwaga maji baharini.

Hatua hiyo inakinzana na maelekezo yaliyomo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 ambayo katika vifungu vya 137 na 139 inaelekeza kuwapo utaratibu maalumu wa kuhifadhi taka hatarishi, zikiwamo za hospitalini.

Sheria hii pia inawapa jukumu Waziri wa Afya na yule mwenye dhamana ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha taka hizo zinachambuliwa na kutunzwa katika kontena maalumu na kuteketezwa kwa utaratibu maalumu.

Mwandishi amebaini utekelezaji wa maelekezo hayo ya kisheria ni hafifu, hivyo kusababisha utupwaji taka ovyo mitaani ambazo baadaye huishia kwenye vyanzo vya maji, zikiwamo fukwe za Bahari ya Hindi, mkoani Dar es Salaam.

Taarifa ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliyochapishwa mwaka 2019, inabainisha kuwa mkoa huo huzalisha taka ngumu, zikiwamo za hospitalini, tani 4,600 kwa siku.

Hata hivyo, taarifa hiyo inabainisha kuwa ni asilimia 6.5 (tani 299) tu ndiyo hurejelezwa, hivyo kuziacha tani 4,301 (asilimia 93.5) zikitupwa ovyo mitaani, ikiwamo mito na hatimaye kuishia kwenye fukwe za bahari.

Vilevile, utafiti uliofanywa na S.V. Manyele (ACHA UZEMBE, SEMA S.V NI NANI?) na wenzake mwaka 2013, ukitathmini mifumo ya usimamizi wa taka za hospitalini katika vituo vya afya vya ngazi za chini (LLHF) katika wilaya za Ilala na Kinondoni mkoani Dar es Salaam, ulionesha kuwa asilimia 83 ya vituo vya kutolea huduma za afya katika Manispaa ya Kinondoni hufukia taka katika mashimo.

Watafiti hao pia walibaini lingine la ziada, kwamba zaidi ya asilimia 50 ya maeneo ya wanakotupa taka hizo hayakuwa na uzio na yalikuwa karibu na makazi ya watu.

"Asilimia 47 ya vituo vya afya katika wilaya za Ilala na Kinondoni hazina taratibu za uendeshaji wa kawaida wa usafirishaji taka za hospitalini.

"Ni changamoto kubwa zaidi katika Manispaa ya Kinondoni ambako asilimia 71 ya vituo vya afya hubeba taka hatarishi kwa mikono wakati wa kwenda kuzitupa, jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya Mazingira," inasomeka sehemu ya ripoti ya watafiti hao.



Sehemu ya taka hatarishi za hospitalini zilizookotwa katika ufukwe wa Rainbow, Manispaa ya Kinondoni na wadau wa mazingira waliokuwa wanafanya usafi kwenye ufukwe huo hivi karibuni. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

Licha ya angalizo hilo la miaka 12 iliyopita, mwandishi wa habari hii amefika kwenye ufukwe wa Raibow, katika Manispaa ya Kinondoni na kukuta taka hatarishi, zikiwamo za hospitalini, zikiwa zimetapakaa pembezoni mwa ufukwe.

Hizo zinajumuisha mabomba ya sindano, dripu, mifuko ya kuwekea dawa na chupa za dawa ambazo baadhi zilionesha muda wa matumizi yake umeshapita, hivyo kuwaweka hatarini kiafya watumiaji wa eneo hilo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Human Dignity and Environmental Care Foundation (HUDEFO), Sarah Pima anasema kuwa kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira, huwa wanafanya usafi katika ufukwe huo mara mbili kwa mwezi, wakikusanya taka, kuzitenga na kuzirejeleza.

Sara anabainisha kuwa kila wanaposafisha ufukwe huo, hukusanya wastani wa tani nne hadi 13 za taka ngumu. Kati yake, asilimia nane ni taka hatarishi za hospitalini.

"Kinachotusikitisha kila tunaporudi kusafisha ufukwe (kila baada ya wiki mbili), tunakuta kiwango kikubwa cha taka kana kwamba hakujafanyiwa usafi kwa muda mrefu," Sara anasema.

Ramadhani Juma anayejitambulisha ni makazi jirani na ufukwe huo, anasema hali ya uchafu katika ufukwe huo imekuwa mbaya zaidi kulinganisha na miaka mitano iliyopita.

"Miaka mitano iliyopita eneo hili lote lilikuwa safi, watu walikuwa wanajaa hapa hadi saa sita za usiku, lakini siku hizi watu wahesabika, wakizidi sana ni 20. Mandhari imeharibika, watu wanahofia afya zao kama wakikanyaga mabomba ya sindano si wanaweza hata kuambukizwa hata VVU?" Juma analalamika.

Mfanyabiashara wa vinywaji katika ufukwe wa Rainbow, Ramadhani Ally anasema uchafu huo umesababisha biashara kuzorota, akifafanua kuwa watu waliokuwa wanakwenda kutembelea na kupunga upepo ufukweni huko wamepungua kutokana na hali hiyo iliyoelezwa na mtangulizi wake Juma.

Anasimulia kuwa awali alikuwa anafanya biashara hadi saa nane usiku kwa kuwa eneo hilo lilikuwa safi na lenye watu wengi, lakini hivi sasa anafunga biashara saa mbili usiku kwa kuwa giza likiingia, watu wanaondoka wakihofia kukanyaga taka na kudhuru afya zao.

"Miaka mitano ya nyuma hapa nilikuwa ninaingiza hadi Sh. 300,000 kwa siku, na duka langu lilikuwa kubwa kuliko lilivyo hivi sasa, lilikuwa limejaa vinywaji, lakini sasa nikiuza sana ni Sh. 50,000 kwa siku.

"Kama unavyoona, duka halina kitu maana hata ukijaza vinywaji vitaisha muda wake wa matumizi vikiwa dukani, unapate hasara, hakuna wanywaji," Ally anasema.

Maimuna Ally anayefanya biashara ya chakula katika ufukwe huo, anasema "kuwapo taka hizi zinazotoa harufu mbaya, ni sababu kuu ya wateja kutukimbia. Biashara yangu imeathiriwa sana. Yaani ninaambulia Sh. 30,000 kwa siku ilhali zamani nilikuwa ninatoka Sh. 100,000 kipindi ambacho ufukwe ulikuwa safi."

Hawa Abdallah naye ana biashara ya chakula katika ufukwe huo. Anasema biashara imekuwa ngumu kutokana na ufukwe kuwa na harufu mbaya aliyoifananisha na harufu ya msalani.

"Yaani ni kama tuko... (anatamka neno lenye maana ya msalani). Upepo ukivuma harufu inasambaa, hali inakuwa mbaya zaidi kwenye eneo hili.

"Si taka za hospitalini tu, bali watu pia huwa wanavizia mvua ikianza kunyesha, wanafungulia mabomba ya vyoo na kutiririsha maji taka. Kama inavyofahamika bahari haikai na uchafu, hivyo madhara yake lazima yanatukumba sisi tuliopo hapa ufukweni," Hawa analalamika.

Daktari Bingwa Mbobezi wa Ubongo, Uti wa Mgongo na Mishipa ya Fahamu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Maxigama Ndosi anasema taka hizo zinaweza kusababisha madhara kwa watumiaji fukwe, ikiwa ni pamoja na kuambukizwa magonjwa hatari kutoka kwa wanyama au wadudu kwa njia ya damu.

Anasema kuwa kama sindano ina kutu, kunakuwa na uwezekano mkubwa mtu kupata tetenasi. Katika hili la kutu, Bingwa Mbobezi Ndosi anatoa angalizo kwamba, kati ya wagonjwa 10 wa tetenasi, sita hufariki dunia.

Bingwa Mboezi Ndosi Alisema sindano hizo hazitupwi na zahanati pekee bali hata watu binafsi baada ya kuzitumia na kuishauri serikali kuweka sheria ngumu kuzuia maduka ya dawa yasiuze sindano kwa wato ovyo bali wale wenye kibali cha daktari.

Dk. Ndosi anasema miongozo inaelekeza taka hatarishi zibebwe katika vyombo maalumu vilivyoandika taka hatarishi na huwa hazitupwi kama taka za kawaida, bali zina utaratibu wake maalumu wa kuzikusanya na kuziteketeza.

"Hata vyombo vyake vya kuzihifadhi huwa vina rangi ambazo zinaonesha ni taka hatarishi ambazo hazipaswi kuhifadhiwa kwa namna ya kawaida," Bingwa Mbobezi Ndosi anasema.

Profesa Philip Bwathondi wa Shule ya Sayansi na Teknolojia ya Uvuvi (SOAF) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) anasema taka hizo zinapotupwa baharini, zinaweza kusababisha madhara kwa viumbe wa baharini kama vile vidonda kwa samaki pale sindano zinapowachoma.

"Athari hizo zipo pia kwa binadamu kwa sababu maradhi yake huwa yaniangia mpaka kwa mlaji wa mwisho ambaye ni binadamu.

"Wadudu wengine wanabeba vimelea kutoka katika hizo taka na mlaji wa mwisho ni binadamu. Katika kila hatua vinapenya mpaka vinafika katika mwili wa binadamu na hatimaye kusababisha maradhi kama vile saratani," anafafanua Prof. Bwathondi.

***USIKOSE KUFUATILIA KESHO KUJUA ZINAKOTOKA TAKA HATARISHI ZA HOSPITALINI ZINAZOTAPAKAA UFUKWENI.**

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Mbowe aahidi mambo saba, Lissu azidi kuwavutia wenyeviti mikoa

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimefanya usaili kwa wagombea wa nafasi mbalimbali kabla ya kwenda kupigiwa kura kwenye Mkutano Mkuu wa Uchaguzi utakaofanyika kesho Dar es Salaam.

Wagombea hao ni wa nafasi za Mwenyekiti Taifa, Makamu Mwenyekiti Bara na Zanzibar pamoja na wagombea wa ujumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA.


Baraza Kuu la chama hicho ndilo limefanya usaili wa wagombea hao. Wagombea wa nafasi ya mwenyekiti ambao walisailiwa jana ni Freeman Mbowe (anayetetea nafasi yake) na ambaye jana alitangaza vipaumbele vyake; Tundu Lissu (Makamu Mwenyekiti Bara) na Charles Odero.

Katika nafasi ya wagombea wa nafasi za Makamu Mwenyekiti kwa Tanzania Bara ni Ezekia Wenje (Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Victoria) na John Heche.

Wengine ambao walifanyiwa usaili hiyo jana ni wagombea wa nafasi ya ujumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho.

**AHADI YA MBOWE**

Wakati huo Mbowe jana alisambaza vipaumbele vyake ambavyo



Freeman Mbowe



Tundu Lissu

anavyotarajia kuvitekeleza ikiwa atachaguliwa tena kuendelea kuongoza chama hicho.

Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni kuunda tume anayoita ya ukweli na upatanisho ndani ya chama hicho ili kutibu majeraha ya uchaguzi wa ndani wa chama hicho na kuhakikisha CHADEMA yote inarudi katika umoja na mshikamano chini ya kaulimbiu yake ya 'Stronger Together'.

Kipaumbele kingine, alisema ni kuboresha, kutanua na kuendeleza utekelezaji programu muhimu za ujenzi na ustawi wa chama na wanachama hususani kuondoa dosari na kuendeleza programu GF na CHADEMA Digital.

Kingine ni kuimarisha CHADEMA Family kwa kuanzisha mfuko rasmi wa kuwezesha wanaCHADEMA kusaidiana na kunyanyuana kiuchumi na kijamii (CHADEMA Family Fund) utakaochangiwa na kusimamiwa na wanachama wenyewe chini ya uangalizi wa chama.

Pia kutanua huduma ya msaada wa kisheria ya ndani ya chama ili kuondoa hofu na kuongeza ujasiri kwa wana-CHADEMA na wananchi katika kupigania na kupata haki zao.

Kipaumbele kingine, Mbowe alisema ni kuamsha vuguvugu kali la madai ya Katiba mpya, Tume Huru ya Uchaguzi na sheria bora za uchaguzi, kwa kutumia nguvu ya umma na kwa kujenga uhusiano na ushirikiano na wadau mbalimbali wa siasa na demokrasia wa ndani na nje ya nchi katika kushinikiza mageuzi chini ya kaulimbiu yao ya 'no reforms, no elections'.

Kadhalika, alisema ataanzisha programu kabambe na endelevu ya kuandaa na kuwawezesha wagombea wa chama hicho kushinda chaguzi, jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya kugharimia sehemu kubwa ya kampeni na ulinzi wa kura katika ngazi zote kwa kuzipatia kipaumbele kikuu.

Mbowe alisema ataanzisha pia programu ya kimkakati na endelevu ya kutoa elimu ya uraia na elimu ya siasa, ili kutengeneza jamii kubwa ya watanzania wenye uelewa mkubwa na ujasiri wa kutosha katika kupigania haki zao za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Uchaguzi wa viongozi hao wa kitaifa wa chama cha CHADEMA utafanyika kesho katika ukumbi wa Mliman City, Dar es Salaam.

**WENYEVITI NA LISSU**

Jana wenyeviti wa mikoa 21 na makatibu wao walikusanyika katika moja ya hoteli zilizoko karibu na Kijiji cha Makumbusho, wilayani Kinondoni na kutoa tamko la pamoja la kumuunga mkono Lissu.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*


**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**PAULINE RICHARD** KAWA anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 195 BLG** aina ya **BOXER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/15699/2025.**


# Lori lingine la mafuta laanguka, dereva mbaroni tuhuma za uzembe

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro linamshikilia Dereva Daniel Mwiluli (39), mkazi wa Makambako, mkoani Njombe kwa tuhuma za uzembe na kusababisha lori alilokuwa anaendesha kupinduka likiwa na mafuta katika eneo la Mzambarauni, barabara kuu ya Morogoro-Dar es Salaam.

Dereva huyo alikuwa anaendesha lori lenye namba za usajili T.257 na Tela T.620 ABG aina ya Howo lililobeba mafuta aina ya dizeli na baada ya kupinduka katika eneo la Mzambarauni, lilizua taharuki huku makundi ya watu wakivamia na kuchota mafuta hayo yaliyokuwa yakimwagika.

Lori hilo lililobeba mafuta ya aina dizeli lita 41,000 limeanguka mita chache kabla ya kufika eneo la Maraha, Msamvu ambako Augosti 10, 2019 ilitokea ajali ya kupinduka lori lililobeba mafuta aina ya petroli na kulipuka moto uliosababisha vifo vya watu 104 na majeruhi wengine kadhaa na kusababisha msiba wa kitaifa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa Morogoro, Alex Mkama alisema tukio la kuangua kwa lori hilo lilitokea mwishoni mwa wiki eneo la Mzambarauni, kata ya Mwembesongo, Manispaa ya Morogoro katika barabara kuu ya Dar es Salaam-Morogoro.

Kamanda Mkama alisema kuwa katika tukio hilo, dereva huyo alipofika eneo hilo aliacha barabara ghafla na kwenda nje ya barabara hiyo na kusababisha lori kupinduka. Hakuna vifo wala majeruhi isipokuwa kiasi kikubwa cha mafuta kimemwagika.

Alisema dereva huyo alikamatwa kusaidia kukamilisha uchunguzi wa tukio hilo na pia alitoa wito kwa madereva wa masafa marefu kupata muda wa kupumzika na kuepuka kuendesha magari wakiwa katika hali ya uchovu, ulevi, msongo wa mawazo au usingizi.

Mratibu Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Morogoro, Daniel Mayalla alisema walipingiwa simu na wananchi majira ya saa 1:24 asubuhi ya siku ya tukio wakieleza hofu yao kutokana na kuanguka kwa lori lililobeba mafuta aina ya dizeli.

Mayalla alisema kuwa baada ya kupata taarifa hiyo, askari wa jeshi hilo walifika eneo la tukio kwa wakati na kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama walifanikiwa kudhibiti tukio hilo na kuwazuia wananchi wasisogelee gari hilo ambalo lilikuwa limebeba mafuta lita 41,000

"Baada ya kufika eneo la tukio, tayari tulikuta mafuta yamewagikia chini na tukanza kuzuia watu wasisogelee, ili kuepuka kuleta madhara zaidi kutokana na tabia ya wananchi kuchukua mafuta kwenye magari ya mafuta," alisema.

Alisema madhara yaliyojitokeza kutokana na ajali hiyo kwa upande wa binadamu ni majeruhi mmoja ambaye ni dereva wa lori hilo na kwa upande wa gari ni uharibifu na upotevu wa mafuta kutokana na kumwagika.

Mayalla alitoa tahadhari kwa wananchi kuacha tabia ya kuchukua mafuta pindi magari yanayobeba mafuta ya aina mbalimbali yanapokuwa yameanguka kwa vile kitendo hicho ni hatarishi kwao wenyewe na wengine.


CSDR Settlement & Custody

**CSD & REGISTRY COMPANY LIMITED**

**KUHAMA KWA OFISI**

Tunapenda kuutaarifu Umma kwamba ifikapo tarehe 20 Januari 2025, Ofisi za **CSD & REGISTRY COMPANY LIMITED (CSDR)** zitahamia katika jengo la Exchange Tower, Morocco Square kama inavyoelekezwa hapa chini:

**Anuani Mpya ya Ofisi:**
**1st Floor, Exchange Tower**
**Morocco Square,**
**Makutano barabara ya Ali Hassan Mwinyi & Mwai Kibaki,**
**Dar es salaam,**
**Tanzania**

Mawasiliano mengine ya simu, posta, barua pepe na tovuti hayajabadilika.

Tunashukuru kwa ushirikiano na tunawakaribisha katika ofisi yetu mpya.

**Mkurugenzi Mkuu,**
**CSD & Registry Company Limited,**
**1st Floor, Exchange Tower, Morocco Square,**
**P. O. Box 70081**
**DAR ES SALAAM**

218329702

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga ikubali kujifunza Simba mechi za maamuzi kimataifa

**KLABU** ya Yanga imeshindwa kusonga mbele kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kumaliza mechi za Kundi A, ikiwa nafasi ya tatu juzi.

Yanga ilimaliza ikiwa na pointi nane na kuziacha MC Alger ya Algeria ikiwa ya pili na pointi zake tisa, huku kinara wa kundi akiwa ni Al Hilal Omdurman ya Sudan iliyomaliza na alama 10.

Katika mchezo huo dhidi ya MC Alger uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, pamoja na kutawala kwa asilimia 69, na kuwaacha wapinzani wao wakiwa na asilimia 31, bado hawakuwa na mbinu mbadala za kuwafungua na kupata angalau ushindi wa bao moja ambao ungewavusha.

Tunadhani bado Yanga haijafahamu jinsi gani ya kucheza michezo kama hii ya kimataifa, ambayo haihitaji zaidi mbwembwe na kutawala mechi, zaidi ya mbinu, mikakati, kujituma na ubinifu wa kupata matokeo chanya.

Katika michuano hiyo, ilionekana Yanga ilitaka kucheza mechi hizo kama inavyocheza dhidi ya Fountain Gate, Dodoma Jiji, KMC, ambapo muda wote inatawala mchezo huku ikisubiri makosa ya wapinzani wao ili kuwaadhibu. Badala yake MC Alger haikutengeneza makosa badala yake ilitengeneza mfumo wa kuzuia ambao ulikuwa mwiba mchungu kwa Yanga.

Tulitegemea kuona Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sead Ramovic, akiwaanzisha Pacome Zouzoua na Clatous Chama katika mchezo huo kwa sababu wanaonekana ni wabunifu na wana uwezo wa kuwafungua wapinzani zaidi kuliko walioanza.

Mechi ya juzi hakuna ambacho Yanga ilihitaji zaidi ya kufunga mabao, hivyo tangu dakika ya kwanza ingekuwa na wachezaji ambao wangeweza kusababisha madhara langoni mwa mpinzani.

Pacome ni mchezaji mwenye uwezo wa kukokota mpira kwa umbali mrefu na kuingia nao ndani ya eneo la hatari, hivyo angesababisha madhara makubwa, pia Chama hana haja ya kuelezewa sana kwani ni mtaalam wa mechi kama hizi za maamuzi, kazi hii akiifanya sana wakati akiwa na timu ya Simba.

Tunaamini katika kusaka maendeleo itakuwa si vibaya kwa Yanga kujifunza kwa timu zilizofanikiwa, na kwa hapa nchini katika michuano hiyo husuan hatua muhimu kama hiyo ya maamuzi kwa mechi ya mwisho ni Simba. Ni kwa sababu wanajua jinsi ya kucheza mechi hizo, wanacheza kwa mikakati, kuheshimu wapinzani na si kwa presha sana.

Ndiyo maana utaona kwenye mechi za maamuzi kama hizo, Simba huanza taratibu na mara nyingi hutanguliwa kufungwa bao, lakini wachezaji wake wanatulia na kurudisha magoli, wakati mwingine kupata na la ushindi.

Kwa misimu saba, Simba imetinga robo fainali sita, nne za Ligi ya Mabingwa na mbili Kombe la Shirikisho, wakati Yanga ikiwa na robo fainali moja Ligi ya Mabingwa na Shirikisho moja.

Desemba 23, 2018, Simba iliifunga Nkana FC mabao 3-1, katika mchezo wa maamuzi ili kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika na msimu huo huo, ilitinga robo fainali kwa kuifunga AS Vita Machi 16, 2019.


2021, Simba iliifunga Al Merrikh ya Sudan mabao 4-1 na kutinga hatua ya robo fainali kwenye mchezo wa maamuzi, iliongoza kundi lililokuwa na Al Ahly ya Misri, Machi 18, 2023, ikaiadhibu Horoya FC ya Guinea mabao 7-0, na Machi 2, 2024, iliichakaza Jwaneng Galaxy mabao 6-0, mechi zote hizo zikiwa ni za maamuzi ya kutinga robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Somo hili kwa Simba walilipata kwenye michezo ya makundi 2019, walipokuwa wakipigwa mabao mengi wakijifanya kucheza kwa swaga, ikapigwa 5-0 dhidi ya AS Vita na idadi kama hiyo dhidi ya Al Ahly.

Hata Mabingwa wa kihistoria wa michuano hii, Al Ahly, siku zote haionekana kucheza soka la kuvutia machoni, lakini wamekuwa ndiyo wanaokwenda kutwaa ubingwa, hapo pia kuna la kujifunza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kocha wa Yanga ana hoja udhaifu Ligi Kuu, asikilizwe

**BAADA** ya Yanga kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kila mmoja anasema lake. Kila mmoja anatoa maoni yake ambayo yeye anadhani yamesababisha kushindwa kuingia hatua ya robo fainali, huku mashabiki wengi wakiitabiria mazuri.

Wengi walitarajia zaidi Yanga kushinda kuliko MC Alger kutoka sare kwenye mechi hiyo ya raundi ya sita hatua ya makundi, timu hizo zikiwa Kundi A.

Moja ya mambo niliyovutiwa nayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, kudai Ligi ya Tanzania ni dhaifu na haizipi timu changamoto kiasi cha kuweza kupambana kwenye michezo ya kimataifa.

Akasema moja ya sababu ambayo timu yake ilikikosa kwenye mchezo dhidi ya MC Alger ni kuhimili kucheza na timu ngumu yenye wachezaji bora, wazoefu, waliotoka kwenye ligi bora, ambao kila wiki wanacheza mechi na timu ngumu.

"Tunapaswa kuwa wakweli kwamba ligi ya hapa Tanzania, ugumu unaokutana nao unapocheza dhidi ya timu nyingine za Tanzania si wa kiwango kikubwa sana. Ukiona ligi za Algeria, Afrika Kusini, Morocco, Tunisia, ni wazi tunahitaji nguvu hiyo ya juu ili kushindana na kuweza kuzoea hali hiyo"

"Ukali wa Ligi ya Tanzania, ni mdogo sana ukilinganisha na nchi hizo, wao ligi yao ni ngumu na kila timu kali sana, tunahitaji ugumu kama wa ligi hizo ili tushindane," alisema kocha huyo.

Hakuna haja ya kufafanua sana alikuwa na maana gani. Ni kwamba urahisi wa kuzifunga timu za Tanzania, huwezi kuupata kwenye michezo ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho.

Hicho ndicho Yanga walichokutana nacho. MC Alger ilionekana waliweza kuikabili na kuhimili vishindo kwa sababu moja tu. Mechi kama hizi wanakutana nazo kwao wiki hadi wiki kwenye ligi yao.

Hapa Tanzania Yanga kupata aina hiyo ya mechi ni pale atakapocheza dhidi ya Simba, Azam, labda kwa sasa Tabora United.

Maneno aliyoyasema kocha wa Yanga yasipuuzwe kwa sababu yana ukweli kwa asilimia nyingi sana hususan kwa upande wa klabu hiyo.

Timu nyingi za Tanzania bado zina madhaifu makubwa, mabeki wanafanya makosa ya ajabu ya kujirudia ambayo yanasababisha timu kubwa zinashinda kirahisi.

Hapo bado, changanya na waamuzi wetu ambao wamekuwa na makosa mengi yanayoitwa ya kibinadamu, nao wanachangia kuifanya ligi kuonekana dhaifu na kutowapa wawakilishi wetu upinzani.

Kama vile haitoshi, wadau wa soka wamekuwa wakipiga kelele juu ya mdhamini mmoja kudhamini timu zaidi ya tano kwenye ligi, kitu ambacho kinaondoa kile kinachoitwa 'fair play' kwenye soka.

Vyovyote itakavyokuwa, hata kama klabu zinahitaji pesa, lakini mdhamini wa kampuni ambayo mpaka inalipa mishahara ya wachezaji wa klabu moja, ikifanya kila kitu kama vile imenunua hisa, kwenda tena kudhamini klabu zingine, huwezi kutegemea upinzani mkubwa kwenye baadhi ya michezo ya ligi kwa timu hizo zinapokutana.

Hata hivyo, hapa kuna cha kujiuliza. Kama ni hivyo ni kwa nini Simba imekuwa ikifanya vema kwenye michezo ya kimataifa kwa misimu kadhaa sasa nchini wakati nayo ipo kwenye ligi hiyo hiyo?

Je, kuwapo kwa ahadi za pesa zinazoahidiwa kila timu inayocheza na Simba ndiyo kunaifanya timu hiyo kuwa imara? Ni jambo la kujiuliza.

Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB) na wadau wote wa soka, wanapaswa kuliangalia hili, kwani huyu si kocha wa kwanza kuongea maneno haya.

Nakumbuka hata kocha wa zamani wa Yanga, aliwahi kubainisha hili. Hawa makocha hawaongei kwa bahati mbaya. Kuna kitu wamekiona. Bahati nzuri kwa sasa nchi yetu ina wachezaji wengi bora kutoka nje ya nchi ambao wamekuwa wakimiminika kucheza soka la kulipwa. Kwa maana hiyo ikiwamo tu dhamira ya dhati, Ligi ya Tanzania inaweza kuwa bora hata msimu huu.

Tatizo ni kwamba soka la Tanzania limekuwa na siasa zaidi kuliko uhalisia ya mchezo wenyewe. Tukiacha siasa na kuacha soka lichezwe kila mechi itakuwa ngumu. Kila wiki timu zetu zitakutana na michezo migumu. Linaweza kabisa kutusaidia huko mbele kwenye michezo ya kimataifa kama Ramovic anavyotaka.

MAKALA

# Utapeli unavvyowaliza watu Mlimani City

Na Halfani Chusi

JANUARI 14 mwaka huu ilikuwa mbaya kwa Christina (jina la pili limehifadhiwa) baada ya kutapeliwa Sh. milioni tisa na aliowaita wauzaji madini feki, akiwa eneo la Mlimani City, mkoani Dar es Salaam.

Akisimulia namna alivyotapeliwa, Christina anasema kuwa siku hiyo alitoka kazini kwake, akaenda kununua mahitaji ya familia eneo la maduka ya Mlimani City, akakumbana na baa hilo ambalo limemsababisha kupoteza fedha hizo.

"Nilipomaliza kununua mahitaji, wakati ninatoka nje nikiwa pale maeneo yanakopaki magari ya wateja, akatokea mama mmoja amejifunga kanga, akiwa anaonekana kama amebeba kitu hivi.

"Akanisalimia akaniambia 'samahani dada nimetoka humo ndani, nilikuwa ninauliza wapi ninaweza kwenda kuuza madini yangu, lakini wamenielekeza kwamba ni huku nje nivuke barabara, ninaomba kama unapajua unielekeze'.

"Nikamwambia sipafahamu, wakati tuko kwenye mazungumzo hayo, akatokea kijana mmoja hivi amevaa suti akaniambia 'huyu mama ana madini halafu anazurura nayo msaidie mwanamke mwenzio asije akatapeliwa, mpeleke pale karibu na Kanisa la Kakobe, kuna dada anahusika na biashara hizo, utaona kuna hospitali imeandikwa Edward'", anasimuliaa huku akibubujikwa machozi.

Christina anasimulia baada ya kuelezwa maneno hayo, aliingiwa na huruma na kumini moja kwa moja mama huyo anahitaji msaada, ikabidi ampeleke.

"Kwahiyo tukaongozana mpaka tukafika pale na kilichonifanya niendelee kubaki pale hata sielewi ni kitu gani, kabla ya kuondoka pale Mlimani City yule mama alimshukuru yule kijana akamwambia akifanikiwa kuyauza yale madini atatugawia Sh. 2,000,000 mimi na yule kijana.

"Yule kijana akasema 'hapana, utatupatia tu Sh. 500,000 ila ya kwangu utaiacha hapo mnapokwenda. Huyu anayekusindikiza (Christina) utampa mkononi kesho kwa sababu ameacha mambo yake kwa ajili ya jambo lako'," anasimulia Christina.

Anasema kabla ya kuondoka Mlimani City, kijana huyo akawa amepiga simu kwa huyo dada atakayewapokea na yule mama mwenye madini akaomba ile namba kisha akampigia kumwambia 'tunakuja akamjibu mkifika hapo, mnisubiri kidogo ninatokea benki'.

"Tukafika karibu na hiyo hospitali tukasubiri kidogo huyo dada akaja akatupeleka moja kwa moja kwenye gari lake akasema huko ndiko kuna kifaa cha kupima hayo madini.

"Tukaingia mimi nikawa nimekaa siti ya mbele yule mama akawa amekaa nyuma, gari lile vioo vyake mtu wa nje hawezi kuona kinachoendelea ndani, akatoa kitu kama kipimajoto, akasema hicho ndicho kinapima madini ikiwaka rangi ya kijani ujue yapo vizuri na ikiwaka nyekundu ujue feki," anasimulia.

Anasema baada ya hapo, akamwambia yule mama ampatie hayo madini ili ayapime kwanza kuona kama yapo sawa, alipompatia akayapima ikawaka taa ya kijani akasema yako vizuri.

Anasimulia baada ya kuyapima akapiga simu kwa mtu aliyemwita kwa jina la Fadher, akaweka sauti ya juu akamweleza kwamba madini ameyaona na ameyapima yako vizuri, akamjibu 'huyo mama tutampa Sh. milioni 200'.



"Baada ya kuongea na huyo Fadher kwa simu akamwuliza yule mama kama ana akaunti ya benki, akamwambia hana. Akaniuliza mimi nikamwambia ninayo, yaani hata sijui nilikuwa nimepumbazwa na nini na sijui ilikuwaje nikakubali.

"Akaniuliza 'ina shilingi ngapi?' Nikamwambia ina Sh. milioni 10. Akaniambia 'hizo fedha ni nyingi kwa sababu tukiongeza na hizo Sh. milioni 150 itaonekana wewe ni mwizi kwa sababu itakuwa imeingia fedha nyingi kwenye akaunti yako.

Kwahiyo chakufanya toa milioni tisa ibaki moja kwenye akaunti yako, ili tuweze kukuingizia hizo fedha halafu Sh. milioni 50 utaibeba tu kwenye pochi'.

Ikabidi nikubali wala sikushtuka kwa lolote! Nikawaambia twende benki Mlimani City ndani nikatoe wakasema twende kwa wakala kule huwa kunakuwa na foleni nikakubali tukaenda kwa wakala wa kwanza tukafanikiwa kutoa Sh. milioni mbili tukaenda kwa wakala wa pili tukatoa Sh. milioni saba tukaziweka kwenye pochi," anasimulia.

Anasema kuwa baada ya kutoa wakarudi katika gari wakamwambia ampatie zile fedha yule mama (muuzaji madini) halafu waongozane kwenda benki ndani Mlimani City, ili akakutane na 'Fadher' ili wamwingizie hiyo fedha katika akaunti yake.

"Kwahiyo tukatoka mimi na huyo dada tukamwacha huyo mama katika gari peke yake, nikiwa nimeshamkabidhi kiasi hicho cha fedha, tukawa tunakwenda benki kwa ajili ya kukamilisha huo muamala, tulipoingia katika jengo hilo karibu na wanapouza piza, yule dada akaniuliza 'umekumbuka kuchukua yale madini kwa yule mama ili tumwoneshe Fadher alipe hizo fedha?'

"Nikamwambia "hapana!" Akasema 'nenda kayachukue' nikamwambia 'twende pamoja', akasema 'nenda tu usijali', tukabishana kwa muda, lakini baadaye nikakubali kurudi peke yangu.

"Looh nimefika pale lile gari sijalikuta, nikakimbia kurudi Mlimani City ndani huyo dada sikumkuta tangu hapo sijawaona tena, ndivyo nilivyotapeliwa, nilipumbazwa!

"Sikumbuka hata kutizama namba ya gari wala hatukubadilishana namba za simu, basi baada ya hapo nikaenda kutoa taarifa Kituo cha Polisi nikapewa RB," anahitimisha simulizi yake.

**MASHUHUDA**

Miongoni mwa wateja wanaokwenda kupata huduma katika eneo hilo, Jamali Nyanganane anasema tukio hilo si la kwanza kutokea eneo hilo.

"Ukiangalia hilo eneo la Mlimani City kuna huduma nyingi za kijamii zikiwamo za kibenki, ni eneo ambalo lina kila aina ya utapeli.

"Ni kama wiki tu imepita, alitokea mama mmoja amepewa dola feki, na aliyemtapeli kwa kujifanya alikuwa anafanya kazi za ndani kwa mchina amelipwa dola hivyo anaomba ampe fedha kidogo ili ampatie zile dola.

"Yule dada alijifanya hawezi kubadili zile fedha, kwa maelezo yake siku hiyo zilikuwa na thamani ya Sh. milioni tatu yeye aliambiwa ampe Sh. milioni 1.5

"Na yeye bila kuwaza alikubali akiamini atakapokwenda kuzibadili atakuwa na faida kubwa alipofika benki akaambiwa dola zote alizokuwa nazo ni feki," anasimulia Nyanganane.

Anashauri kamera za ulinzi katika eneo hilo ziongezwe ili linapotokea tukio kama hilo na mengine iwe rahisi kufuatilia kumkamata mtuhumiwa.

"Wanaotapeli wanakuwa hawajavaa kitu chochote cha kuficha sura, hivyo kamera katika eneo lile ziongezwe, ninadhani hiyo itasaidia kuwakamata wanaojihusisha na vitendo hivyo.

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro anathibitisha kuwapo matukio hayo, akieleza kuwa kwa sasa yamepunguza kulinganisha na kipindi cha nyuma. Wengi wanatapeliwa kwa sababu ya tamaa.

"Tumekuwa tunatoa elimu mara kwa mara, lakini watu si wasikivu, ukiona unashawishiwa kupata fedha nyingi kwa mara moja, shtuka! Huo ni mtego.

"Tumetoa elimu na elimu kuanzia kwa wale wa 'tuma kwenye namba hii', wanaofanya hivyo kwa kutumia njia ya madini, na mambo ya dola kwenye mitandaoni huko tumeshaelimisha sana," anasema Kamanda Muliro.

Anasema watu wengi huwa wanaingia katika mtego huo, wakidhani watapata zaidi, mwisho wa siku wanaishia kutapeliwa.

Anasema wengi wanaofanya utapeli wa namna hiyo, huwa wanakuwa zaidi ya wanne na wote wanakuwa lao moja japo kwa namna wanavyoigiza unaweza kudhani kama si watu wanaofahamiana.

Kamanda Muliro anashauri watu wanapokutana na hali hiyo, wajaribu kuwaza zaidi ya mara mbili, hata kwa kutumia hesabu za kufikiria, akihadharisha "ukiona mtu anakuletea dili mezani ambalo linakupa faida kubwa kwa mara moja, jua hapo unatapeliwa".

Anasema wapo wengi waliokamatwa na kufikishwa katika vyombo vingine vya sheria ikiwamo mahakamani, huku akionya wanaotapeli watu kuacha kwa kuwa ni kinyume cha sheria na atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***





Mkuu wa Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Naitapwaki Tukai (watatu kushoto), akiwa na baadhi ya wazazi na walezi wa watoto yatima na wenye uhitaji maalum baada ya kuwakabidhi msaada wa vifaa vya shule, ofisini kwake juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# CCM yamtega Mkurugenzi Ilala mgogoro wa ardhi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ilala, Mtiti Jilabu, amemtaka Mkurugenzi wa Jiji hilo, Heri Huruma kushughulikia haraka mgogoro wa ardhi ulioibuka katika eneo lililoko kati ya Shule ya Msingi na Sekondari Zavala, jijini ambalo linadaiwa mmiliki wake halali alikuwa George Chawala.

Mgogoro huo umeibuka baada ya mmiliki wa sasa wa eneo hilo, Shabani Mapelele, maarufu Mapete, kulinunua kutoka kwa Chawala; naye akapima viwanja na kuwauzia watu mbalimbali ambao wameanza kujenga makazi ya kudumu.

Akizungumzia uhalali wa eneo hilo, Mapete alidai kuwa alilinunua kutoka kwa Chawala miaka mitatu iliyopita; naye Chawala alilinunua kwa Musa Nyemba mwaka 2000 kulingana na hati ya mauziano aliyoitoa mnunuzi wa pili.

Mtiti amelazimika kumtaka Mkurugenzi Huruma kutolea tamko suala hilo kwa kuwa ndiye mwenye mamlaka na maeneo ya shule ambazo zimo jijini humo.

Katibu huyo wa Wazazi CCM Ilala alibainisha kuwa baada ya kuzuka mgogoro huo, alikwenda katika eneo hilo ambako baadhi ya wakazi na viongozi wanadai eneo hilo ni la Chawala kwa kuwa hakufidiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) na wengine wanadai eneo hilo ni mali ya shule.

Mwaka 2009, TAA walithaminisha mashamba ya wakazi wa eneo hilo kupitia mradi wake wa kuhamishia watu wa Kipawa ambao walihamishwa kwa ajili ya kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), jijini Dar es Salaam.

Mjumbe wa Shina Na. 4 la CCM eneo zilikojengwa shule hizo, Denis Masombola, ambaye pia ni mlinzi wa shule hizo hadi sasa, alidai kuwa eneo hilo liliachwa katikati kwa kuwa Mzee Chawala hakuwa amelipwa fidia.

Akizungumzia mgogoro huo, aliyekuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Zavala, Chiku Mwalutambi, alithibitisha kwa vielelezo kuwa eneo hilo ni la George Chawala kwa sababu hakufidiwa.

**Mmoja wa wakazi wa Kisegese, Rukia Msumi (80), alidai wamechoshwa na alichokiita "kunyanyaswa na viongozi wa tarafa na kata ambao wanataka kumega ardhi yao ili ichukuliwe na kijiji jirani...**

Chiku alidai kuwa kutokana na Chawala kutolipwa fidia na mamlaka husika, wakati wanaanza kujenga shule hizo walilazimika kujenga kwenye maeneo yaliyolipwa na kuliacha hilo la katikati.

Mwenyekiti wa CCM Tawi la Zavala, Nassoro Msangawina, alikiri kwamba George Chawala ni miongoni wa watu ambao hawakulipwa fidia na TAA.

Diwani wa Buyuni, Athuman Maembe, alidai kuwa kuliwahi kuzuka madai miongoni mwa wananchi wa eneo hilo yaliyozua mkanganyiko kuhusu uhalali wa umiliki wa eneo hilo.

Maembe alifafanua kuwa wakati wa mkutano wa wananchi wa mtaa huo ambao naye alishiriki, Chawala aliitwa na kuonesha vielelezo vya umiliki halali wa eneo hilo, lakini anashangaa kuona mgogoro huo unaibuka tena huku wanaodai wakikosa ushahidi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Zavala aliyeingia madarakani hivi karibuni, Faridu Sadiki alisema hajui mmiliki halali wa eneo hilo.

Ofisa Habari wa TAA, George Lupatu, akijibu hoja zilizoelekezwa kwake iwapo Chawala alilipwa fidia, alisema viongozi wengi wako safarini jijini Dodoma, akiahidi watatoa majibu wakishaerejea.

Hata hivyo, baada ya madai hayo mwandishi wa habari hizi alikwenda mara nne tofauti ofisini kwa Mkurugenzi wa Jiji la Ilala, Heri Huruma kutaka kupata ukweli wa madai hayo bila mafanikio.

Mara ya kwanza Huruma alisema kuwa yeye si mzungumzaji, taratibu za serikali kwa sasa zinaelekeza kuwa anayetakiwa kuzungumzia madai mbalimbali ni Ofisa Habari wa Jiji.

Alipokwenda ofisi ya Ofisa Habari wa Jiji, Tabu Shaibu, mwandishi aliambiwa kuwa alikuwa likizo ya sikukuu za mwisho na mwanzo wa mwaka, alitarajiwa kurejea ofisini Januari 6, mwaka huu.

Baada ya tarehe hiyo, mwandishi alirudi tena ofisi ya Ofisa Habari huyo, alikutana na Kaimu Ofisa Habari ambaye alimwambia alirudi siku nyingine, atawapigia simu wakuu wa vitengo vinavyohusiana na ardhi ili watoe ufafanuzi, lakini alidai kukosa ushirikiano kutoka kwa wakuu hao.

Mara ya Tatu mwandishi alirudi tena kwa mkurugenzi ambaye alimtaka amsubiri Tabu atakapokuwa amerudi kutoka likizo kwa kuwa anafahamu mambo mengi kutokana na uzoefu alionao kazini.

Baada ya kurrejea kwa Tabu, alisema hawezi kuzungumzia suala hilo na kumtaka mwandishi ampe muda aonane na wakuu wa vitengo vya ardhi.

Hata hivyo, aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji Ilala, Jomaary Satura aliwahi kuzungumzia suala hilo kabla hajahama jijini Ilala, akisema eneo linakuwa la serikali ikiwa aliyekuwa analimiliki amelipwa fidia, kinyume chake ni la mwananchi mwenyewe.

Satura alitoa ufafanuzi huo alipoulizwa kuhusu mgogoro huo ulipozuka mwanzoni mwa mwaka jana.

Mtoto wa marehemu, George Chawala, Johnson, alisema eneo hilo ni la baba yake kwa sababu hakulipwa fidia na mamlaka husika kama ilivyokuwa kwa watu wengine aliopakana nao.

Johnson alisema baba yake alinunua eneo hilo mwaka 2000 kutoka na Musa Nyemba.

Mtoto huyo wa Chawala ambaye alimwonesha mwandishi wa habari nyaraka za mauziano kati ya baba yake na Nyemba, alidai alinunua shamba la ekari mbili kwa makisio wakati huo eneo hilo likiitwa Buyuni Vikurunge.

Alisema kuwa baadaye shamba hilo alimwuzia mfanyabiashara anayeuza viwanja, Shaban Mapelele.

# Ripoti: Huduma za intaneti nyumbani, ofisini zaimarika

**Na Mwandishi Wetu**

HUDUMA za intaneti kupitia waya za faiba zilizounganishwa majumbani na ofisini na kasi yake zinazidi kuongezeka nchini, hali inayoashiria mwelekeo mpya wa utumiaji teknolojia zinazojumuisha watu wengi.

Hayo yanabainishwa katika Ripoti ya Hali ya Mawasiliano Tanzania ya Desemba 2024 iliyotolewa hivi karibuni na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanznaia, Dk. Jabiri Bakari.

Alisema ingawa teknolojia za faiba nyumbani (FTTH) na ofisini (FTTO) hazijaenea sana nchini, zina kasi karibu mara tatu ya teknolojia za simu za vifaa vya mkononi.

"Kasi ya teknolojia zinazowezesha intaneti inapitia kipimo cha megabaiti kwa sekunde (Mbps)," ilifafanua ripoti hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, laini 48,028,227 zilitumika kwa huduma za intaneti Desemba 2024, huku laini za FTHH zilikuwa 71,660 na FTTO 11,540 na zilizobakia zilitumia njia ya simu za mkononi. FTTO zina idadi ndogo ya laini 71,661 na 11,540 mtawalia.

"Huduma ya intaneti zinatolewa kupitia laini za simu, waya (faiba) na mawimbi. Idadi ya utumiaji intaneti inatokana na laini/waya ambazo zimetumia huduma ya intaneti angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita bila kujali teknolojia iliyotumika," mkurugenzi huyo alisema.

Mkurugenzi huyo alisema idadi ya utumiaji wa intaneti imeongezeka kwa asilimia 16 kutoka milioni 41.4 kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 hadi milioni 48 kwa robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024.

"Simu 56,862,95 za kawaida au simu rununu na 23,419,299 zenye uwezo mkubwa, maarufu simu janja zilitumika mitandaoni Desemba 2024.

"Kasi ya kupakua data kwa teknolojia ya vifaa vya mkononi ilikuwa Mbps 10.8, wakati kwa teknolojia ya FTTH ilikuwa 31.8 Desemba 2024. Ilikuwa 13.2 na 40,9 mtawalia Septemba mwaka jana," inafafanuliwa katika ripoti hiyo.

Alisema hadi Desemba 2024 huduma za FTTH na FTTO zilitolewa na kampuni 48 zilizo na leseni ya TCRA ya programu tumizi za mawasiliano.

"Usajili wa intaneti ya waya wa faiba unajumuisha usajili wa mtu binafsi na wa taasisi. Teknolojia ya FTTH inawezesha watu wengi zaidi kwenye eneo ilipofungwa kupata huduma kwa mtandao unaowezesha watu wengi kujiunga na chombo kimoja kilichounganishwa," alisema.

Vilevile, inatoa fursa ya watumiaji kupata huduma nyingi zaidi zikiwamo filamu na burudani nyingine wakiwa majumbani.

"Wastani wa matumizi kupitia laini hizo ilikuwa ni gigabaiti (Gb) 4.49 kwa laini, ikiwa ni juu ya Gb 4.35 Septemba, uchambuzi wa ripoti umethibitisha," alisema.

Alisema pamoja na laini zinazotumia intaneti kuongezeka kutoka 46,084,364 Oktoba hadi 48,028,227 Desemba 2024, ripoti hiyo inasema watumiaji intaneti wanatumia asilimia 10.9 ya uwezo wa kuunganisha huduma ya intaneti kwenda nje ya Tanzania na kuingia nchini.

"Tanzania ina uwezo wa Gigabaiti kwa sekunde (Gbps) 17,200.00 kwa ajili ya uunganishaji huduma ya Intaneti ambako 1,868.32 tu ndizo zilitumika Desemba 2024. Kuna 15,331.68 zinazosubiri kuunganishwa," alisema.

# Uchunguzi kesi ya maofisa wa ROMBOWSSA waiva

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

UCHUNGUZI wa kesi ya rushwa inayowakabili watumishi wawili wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Wilaya ya Rombo, mkoani Kilimanjaro, (ROMBOWSSA) umeiva.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mkoa wa Kilimanjaro, Musa Chaulo, alisema wakati wowote kuanzia sasa watumishi hao watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Kwa mujibu wa Chaulo, taasisi hiyo inawashikilia watumishi wawili wa mamlaka hiyo, kwa kuomba rushwa ya Sh. 550,000 kwa mteja ambaye walibaini mita yake (dira ya maji) ina changamoto.

Wanaoshikiliwa wakikabiliwa na tuhuma hizo ni Fredrick Kiwango na Lucas Malaba.

Inaelezwa kuwa Desemba 31, mwaka jana watumishi hao wakiwa katika majukumu yao ya kawaida ya ukaguzi walibaini kuna dira ya mteja wao ina changamoto iliyosababishwa na mteja huyo.

Baada ya kubaini hilo watumishi hao wa ROMBOWSSA walimchukua na kuondoka naye ambapo walimtaka mteja huyo atoe faini ya Sh. milioni 1.5

Alisema baadaye waliongea na mteja huyo na kumshawishi awape Sh. 550,000 ili wamalizane naye na mteja huyo aliwasilisha malalamiko yake TAKUKURU na kuwawekea mtego uliowanasa.

Alisema: "Waliongea na huyo mteja na kumshawishi alipe shilingi 550,000 ili hilo suala liweze kumalizika. Januari 10 mwaka huu mteja huyo aliwasilisha malalamiko yake kwetu na sisi tuliandaa mtego na kuwakamata wahusika".

# Mradi nishati safi wa bil.1/- waiva

**Na Godfrey Mushi,** MONDULI

MRADI wa nishati safi wa restore, wenye thamani ya Sh. bilioni moja unatarajiwa kutekelezwa katika wilaya za Babati, (Manyara) na Monduli (Arusha), wakati wowote kuanzia sasa.

Lengo la kuanzisha mradi huo maeneo hayo ni kuongeza matumizi ya nishati safi na kukuza uchumi wa maeneo hayo hasa katika sekta ya utalii.

Akizungumza kuhusu utekelezaji wa mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Festo Kiswaga, alisema serikali itazingatia vigezo vya walengwa wakati wa utekelezaji ili kuhakikisha yanakuwepo mafanikio makubwa.

Mradi huo pia unalenga utunzaji wa mazingira kwa kupunguza matumizi ya nishati chafu kwa asilimia kubwa. Kiswaga alisema zaidi ya kaya 300 zitanufaika na mradi huo kupitia matumizi ya majiko banifu na mitambo ya nishati ya jua, huku vijana 48 na wanawake 80, wakipata ajira katika utengenezaji wa majiko na ufungaji wa mitambo ya sola.

**Januari 16 mwaka huu serikali ilisema inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia ili kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato ...**

Januari 16 mwaka huu serikali ilisema inaendelea na ukamilishaji wa taratibu za kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia ili kuweka ruzuku itakayowawezesha wananchi wa kipato cha chini kumudu bei ya gesi.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kanuni za usimamizi wa miradi ya biashara ya kaboni zinabainisha ruzuku kupitia hakimiliki za kaboni zinazopatikana kutokana na kupunguza matumizi ya nishati inayochafua mazingira.

Hivyo, ruzuku hiyo ni sehemu ya juhudi za kitaifa za kutekeleza malengo ya kupunguza gharama kwa watumiaji wa nishati safi.

Katika jitihada za kupunguza gharama za matumizi ya nishati mbadala, serikali imesaini makubaliano ya awali na wawekezaji kuhusu ruzuku ya Sh. bilioni 8.64 kwenye nishati safi ya kupikia mbapo jumla ya majiko 452,455 yamepata ruzuku.



Mafundi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, wakibeba bomba la maji ili kulipakia kwenye gari kwa ajili ya kwenda kusambaza huduma ya maji kwa wananchi, wilayani humo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Jela miezi miwili kwa kuiba mita za maji

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Mwanzo Babati imewahukumu kwenda jela miezi miwili wafanyabiashara wawili wa vyuma chakavu wilayani Babati mkoani Manyara.

Washtakiwa hao walihukumiwa kifungo hicho baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kuiba mita ya maji ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Babati (BAWASA) na vifaa vingine vya maji.

Adhabu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na hakimu wa mahakama hiyo, Kangida Kalembo.

Katika hukumu iliyosomwa Hakimu Kalembo alisema wanaotumikia adhabu hiyo ni Abubakar Sembuli (18) na Abdul Hamza (18).

Kalembo alisema washtakiwa hao waliharibu mali kinyume na Sheria ya Mali, Kifungu cha 326 (1), Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Alisema washtakiwa walikamatwa Desemba 24 mwaka jana, majira ya saa 1:45 asubuhi maeneo ya Maisaka wakiwa ofisini kwao, ambapo walikutwa na mita ya maji ya BAWASA kwenye vyuma chakavu wanavyonunua.

Aidha, Hakimu Kalembo alisema kwa upande wa utetezi ziliwasilishwa hoja tatu zikionyesha kuwa washtakiwa walifanya uharibifu kwa makusudi.

Mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo, Abubakari Sembuli, alipopewa nafasi ya kujitetea ili apunguziwe adhabu, alidai kuwa mama yake ni mjane na wadogo zake wanamtegemea kuwasaidia.

Wakati mshtakiwa wa pili, Abdul Hamza, alidai yeye anayo familia ya watoto wawili na wote wanamtegemea.

Nje ya mahakama baada ya hukumu hiyo, Meneja Huduma kwa Wateja wa BAWASA, Rashid Charahani, aliishukuru mahakama kwa kutenda haki.

Meneja huyo alidai kuwa mita za maji huwa zinaibiwa kwa wateja, hivyo walipofanya ukaguzi walikuta mita kwa wauzaji wa vyuma chakavu.



# HABARI KANDA YA ZIWA

# Mfanyabiashara awapa mbinu TRA ukusanyaji mapato

**Na Vitus Audax**

MFANYABIASHARA na mmiliki wa kiwanda cha sabuni mkoani Mara, Judith Lugembe, ameishauri serikali kupitia Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi kutazama upya njia zinazotumika na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukusanya kodi na kueleza kuwa njia zilizopo zimepitwa na wakati.

Judith alibainisha hayo juzi katika kikao baina ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi na wadau wa kodi wa Mkoa wa Mara kilichofanyika katika Manispaa ya Musoma ikiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Tume, Balozi Maimuna Tarishi.

Alisema kwa sasa maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wamekuwa wakiwalipisha kodi kwa kukadilia akiita hatua hiyo kuwa ni kufanya kazi kwa mazoea, akidai kuwa wafanyabiashara wengi hawalipi mapato halisi serikalini na badala yake wanatoa rushwa ili wapewe makadirio kidogo ya kodi.

Alisema serikali inatakiwa kuona umuhimu wa wafanyabiashara kufungua akaunti za biashara na kodi zao kukatwa katika akaunti hizo kulingana na mapato na matumizi ya kampuni hizo.

Kadhalika aliiomba serikali kuangalia kampuni zinazotoa mashine za EFD kwani zinakuwa kero kwa wafanyabiashara kutokana na kukatwa fedha za kuinunua upya kila mwaka kwa Sh.145,000.

**"Tunaomba pia serikali iunde Kamati ya Ushauri ya Kodi ya Mkoa ambayo itashughulikia matatizo ya kikodi yanayotukabili wafanyabiashara..."**

"Tunaomba pia serikali iunde Kamati ya Ushauri ya Kodi ya Mkoa ambayo itashughulikia matatizo ya kikodi yanayotukabili wafanyabiashara katika mkoa husika kuliko utaratibu uliopo wa mfanyabiashara kutakiwa kukata rufani ya kikodi," alisema Judith.

Makamu Mwenyekiti wa Tume hiyo, Balozi Maimuna Tarishi aliwataka wananchi na wadau wa kodi kuendelea kutoa maoni yao kupitia mifumo mbalimbali iliyowekwa na tume hiyo ili kuweza kusaidia katika maboresho ya mfumo wa kodi unaofaa kutumika nchini.

Balozi Tarishi alisema tume hiyo imejipanga kuwafikia watu wengi Tanzania Bara na Zanzibar ili kupata maoni, kero, changamoto na mapendekezo yao kwa kuzungumza nao kwa njia ya ujumbe wa simu za mkononi, barua pepe, dodoso la mtandaoni na tovuti ya tume hiyo.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Khalfan Haule aliwashukuru washiriki wa kikao hicho kwa kutoa maoni ambayo yanaenda kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa kodi na kuwataka waendelee kushiriki kutoa maoni kupitia kwenye mitandao kama walivyoelekezwa na tume hiyo.

Tume hiyo iliundwa na Rais Samia Suluhu Hassan Oktoba 4, 2024 ili kuandaa mapendekezo ya namna bora ya kuboresha mfumo wa kodi nchini baada ya serikali kupokea kwa nyakati tofauti malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusiana na kodi.

Miongoni mwa majukumu ya tume hiyo inayoongozwa na Balozi Ombeni Sefue, Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu ni pamoja na kuchambua sera na sheria za kodi na kubaini maeneo ya kuboresha, athari za viwango vya kodi katika sekta ya uchumi, kufanya mapitio ya mifumo na mbinu za ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, kuchambua usimamizi na utekelezaji wa sheria za kodi, kuchambua mapato yasiyo ya kodi yanavyoathiri sekta za uzalishaji.

Kadhalika inatakiwa kuainisha changamoto zinazoathiri utendaji wa mamlaka zinazosimamia ukusanyaji wa kodi, ushuru, tozo na ada mbalimbali, kuchambua usimamizi wa mapato ya mamlaka za udhibiti na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kupokea na kuchambua maoni ya wananchi na wadau, kupata uzoefu kutoka kwenye nchi nyingine kuhusu masuala ya kodi na kuandaa taarifa jumuishi.



Mfanyabiashara Gilitu Makula, akitoa malalamiko yake kuhusu utitiri wa kodi kwa wafanyabiashara ikiwamo na kodi ya ushuru wa huduma ambayo inatozwa ndani ya mtaji na siyo faida, wakati wa Mkutano wa Tume ya Rais ya uboreshaji mifumo ya kodi, mjini Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Diwani ataka 'korokoro' zitozwe ushuru

**Na Alex Sayi,** MASWA

DIWANI wa Kata ya Seng'wa, Dese Mohamed ameishauri Halmashauri ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu kukusanya ushuru katika michezo ya bonanza maarufu kama 'korokoro' kutokana na kuzidi kuongezeka bila kutumiwa kama sehemu ya mapato.

Alitoa ushauri huo juzi wakati wa kuidhinisha na kupitisha makadirio ya bajeti ya zaidi ya Sh.bilioni 47.2 ya mwaka 2025/26 kwenye Baraza la Halmashauri hiyo.

Pamoja ukusanyaji wa mapato kwenye michezo ya bonanza, vilevile alisema kuna haja ya kutoa vipaumbele upande wa ngoma za jadi na mpira wa miguu ikienda sambamba na uboreshaji wa viwanja vyake.

Naye Diwani wa Kata ya Ng'wigwa, Steven Dwese aliishauri halmashauri hiyo kuwekeza kwenye miundombini ya kuhudumia mifugo ikiwemo ujenzi wa majosho na uchimbaji wa mabwawa ya kunyweshea mifugo kutokana na kutegemea kwa kiasi kikubwa mapato kwenye kilimo na mifugo.

Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Julius Ikongora akiwasilisha Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26 kwa niaba ya Mkurugenzi alisema bajeti hiyo inaongezeko la zaidi ya Sh.milioni 379.9 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2024/25 ongezeko litokanalo na makusanyo ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Alisema bajeti hiyo imejielekeza zaidi kwenye vipaumbele vya ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya, kuboresha hali ya lishe na uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo, upimaji wa afya ya udongo na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji.

Alisema: "Itasaidia kukabiliana na changamoto ya upungufu wa madarasa ambayo ni 994 madawati, viti na meza,13,656 na upungufu wa matundu ya vyoo 3,793".

# Mbunge ataka ushirikiano kuinua uchumi, umaskini

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MBUNGE wa Tarime Mjini, Michael Kembaki amewataka kinamama na vijana kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo, ili waweze kuinua uchumi wao na kuondokana na umaskini.

Alitoa ushauri huo juzi alipofanya ziara ya kutembelea vikundi mbalimbali vya uzalishajimali sambamba na kuwapatia Sh. milioni 4.9 kwa ajili ya kuwezesha vikundi hivyo vinavyonufaika na mkopo wa asilimia 10 kutoka Halmashauri ya Mji wa Tarime.

Kembaki alisema katika kushirikiana wanaweza kuboresha shughuli zao na kuzalisha zaidi ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema msaada aliioutoa utawezesha wasimamizi wa vikundi hivyo kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi zao ili waweze kuwa na sehemu za kuratibu na kufuatilia shughuli zao za kila siku.

"Nimetumia fedha za mfuko wa jimbo zaidi ya Sh.milioni 45 kwa miaka minne iliyopita kuwezesha vikundi kadhaa vya kinamama na vijana ambao wengi wamenufaika na mkopo wa halmashauri ili waweze kukuza mitaji yao kwa umoja wao wenyewe," lisema Kembaki.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Mji wa Tarime, Vitus Gwanko alisema serikali imekuwa ikiviwezesha vikundi ili kujikukza kiuchumi ambapo hadi sasa vikundi 457 vimesajiliwa katika eneo hilo.

Alisema halmashauri hiyo inachukua hatua kutoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa wanachama ili kuzuia matumizi mabaya ya rasilimali na kuwawezesha kurejesha mikopo yao kwa wakati.

Alisema: "Divisheni ya maendeleo ya jamii inaendelea kutoa elimu kwa wanawake na vijana waendelee kujiunga na vikundi vya kijamii ili kuharakisha maendeleo kwa taifa na ustawi wa jamii".

Nipashe
Spotika



FOWADI 6 WANAOWEZA KUMRITHI JESUS ARSENAL UK. 12-13



# KLABU ANAZOWEZA KUTUA RASHFORD

**MANCHESTER,** England

KWA Marcus Rashford, Januari hii anaweza kudhibitisha mwezi ambao unafafanua maisha yake yote.

Winga huyo wa Manchester United amezungumzia hadharani nia yake ya kutaka changamoto mpya baada ya kutumia maisha yake Old Trafford na inaonekana kwamba matakwa yake yatatimizwa kabla ya mwisho wa dirisha la msimu huu wa baridi.

Uhamisho wa mkopo unaonekana uwezekano zaidi kuliko mauzo ya kudumu jinsi mambo yanavyoendelea.

Inaeleweka, Rashford mwenye umri wa miaka 27, ana orodha pana ya klabu zinazomtaka. Ingawa kiwango chake kimeshuka katika kipindi cha miezi 18 iliyopita, Rashford alifunga mabao 30 msimu wa 2022/23, akiwa amefunga zaidi ya 20 katika misimu miwili kati ya mitatu kabla ya hapo.

Wanunuzi watarajiwa wanaweza kuvunja benki kwa ajili ya kuwania saini ya mchezaji huyo. Kwa kuzingatia hilo, hapa kuna maeneo yanayowezekana Rashford akatua huko kucheza.

### Como

Wapinzani walioshangaza kupata saini ya Rashford kwa mkopo ni Como ya Italia, ambayo ilipandishwa Serie A kwa mara ya kwanza baada ya miaka 21 kabla ya kampeni ya sasa. Kwa sasa wanapambana kutoshushwa daraja chini ya Kocha Cesc Fabregas, huku kunusurika kukiwa mbali sana na kuelekea kipindi cha pili cha muhula huo.

Rashford bila shaka angekuwa samaki mkubwa katika bwawa dogo huko Lombardy, haswa baada ya mchezaji mwenzake wa zamani, Raphael Varane kustaafu mnamo Septemba baada ya kujiunga na Como msimu wa majira ya joto. Itatoa muda wa uhakika wa mchezo na matarajio machache.

### Tottenham Hotspur

Man Utd hawana uwezekano mkubwa wa kumtoa Rashford kwa adui wa moja kwa moja - wanaweza kuwa wamejifunza somo baada ya kumpeleka Jadon Sancho Chelsea, ambapo winga huyo anatamba - lakini 'Mashetani Wekundu' na Tottenham hawashiriki mchuano mkali.

Spurs wako katika msako wa kuongeza nguvu msimu huu wa baridi, huku Rashford akiwa miongoni mwa wanaozingatiwa. Tottenham wana nia ya kuimarisha safu yao ya mbele - hata kama safu yao ya ulinzi inahitaji damu safi - na kocha Ange Postecoglou atakuwa kocha wa kuvutia kwa wachezaji wengi washambulia.

Rashford, ambaye amefunga mabao sita katika mechi 17 alizocheza dhidi ya Spurs, angepewa nafasi ya kushambulia zaidi Kaskazini mwa London, ingawa atakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa Son Heung-min kwa nafasi ya kuanzia kwenye safu yake ya kushoto anayopendelea.

### Napoli

Rashford anaweza kuwa amesikia hadithi za kutisha za Antonio Conte kutoka kwa marafiki na wachezaji wenzake, lakini anaweza kuwa na nafasi ya kumwona Muitaliano huyo katili kwa muda uliosalia wa kampeni. Napoli, ambao wameongoza kwenye kilele cha Serie A chini ya kocha huyo wa zamani wa Chelsea na Spurs, wanawinda saini yake.

Kuvutiwa kwao na Rashford kumeongezeka baada ya kuondoka kwa supastaa wao, Georgia Khvicha Kvaratskhelia, ambaye amejiunga na PSG.

### Juventus

Ukosefu wa uzoefu wa Juventus katika maeneo mengi ya ushambuliaji umethibitisha tatizo kwa Kocha Thiago Motta wakati wa kampeni yake ya kwanza mjini Turin. 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kilijihami kwa muda huu, lakini kimekosa ustadi, uthabiti na cheche upande mwingine wa uwanja.

Kwa kawaida, wanatafuta suala hilo Januari hii, huku Rashford akiwa miongoni mwa malengo yao. Chaguzi za sasa za fowadi wa Juve hazina msukumo, huku hata nyota Dusan Vlahovic akijitahidi kuwashawishi miamba hao wa Uwanja wa Allianz.

### Borussia Dortmund

Borussia Dortmund mara nyingi wametoa hifadhi kwa Waingereza. Jude Bellingham na Jadon Sancho walifanya vema kwenye Uwanja wa Signal Iduna Park, na hivyo kupata matokeo aliporejea msimu uliopita kwa mkopo kutoka Man Utd. Hata ndani ya kikosi chao cha sasa, Jamie Gittens anafurahia kampeni kali.

Hadithi kama hizo rasilimali kama msukumo kwa Rashford, ambaye angekuwa akifanya kazi chini ya kocha mchanga anayesisimua Nuri Sahin. Sancho alijenga upya heshima yake akiwa na wababe hao wa Bundesliga msimu uliopita na kufika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na kuruhusu kujitengenezea njia kuelekea Magharibi mwa London majira ya kiangazi yaliyopita.

### AC Milan

Huenda ikawa haraka kutaja timu za Italia ambazo zinataka kumsajili Rashford msimu huu wa baridi, huku AC Milan ikiongoza mbio hizo. Walikuwa timu ya kwanza kufanya mbinu rasmi kwa Man Utd, huku mabingwa wa hivi majuzi wa Supercoppa wakitaka kujiimarisha tena chini ya kocha mpya, Sergio Conceicao.

Wawakilishi wa Rashford wameripoti kuhusu kuhamia Milan baada ya kutumwa kwenda Italia, na mkataba wa mkopo ukijumuisha chaguo la kumnunua kulingana na mahitaji ya mshahara.

Rashford angekutana na watu wengine wanaofahamika huko Milan kwani Waingereza watatu Ruben Loftus-Cheek, Tammy Abraham na Fikayo Tomori wote wanawawakilisha Rossoneri. Hiyo hakika ingesaidia kutulia katika mchakato.

## ISIKUPITE



HAT-TRICK aliyoifunga Mshambuliaji wa Bournemouth, Justin Kluivert dhidi ya Newcastle United katika Uwanja wa St James' Park, juzi kwenye mechi ya Ligi Kuu England wakishinda 4-1, inamfanya kuvunje rekodi ya mabao ya baba yake, Patrick Kluivert, katika uwanja huo, ambaye enzi akiichezea Bournemouth alifunga bao moja tu uwanjani hapo. Patrick aliitumikia klabu hiyo msimu wa 2004/05 na kufunga jumla ya mabao 13 katika mechi 37 alizocheza.

Extra Time

# FOWADI 6 WANAOWEZA KUMRITHI JESUS ARSENAL



ISAK

**LONDON,** England

ARSENAL imejikuta katikati ya dirisha la usajili la Januari huku eneo moja la kikosi chao likihitaji kuongezewa nguvu.

Kutokana na majeraha ya muda mrefu ya Bukayo Saka na Gabriel Jesus, ambaye aliumia misuli ya nyama za paja katika kichapo cha wikiendi moja iliyopita kutoka kwa Manchester United kwenye Kombe la FA, Arsenal italazimika kufikiria kuimarisha safu yao ya ushambuliaji wakati wa dirisha la majira haya ya baridi.

**'Washikabunduki' hao wamekuwa na wakati mgumu wa usajili kwa kushindwa kumsajili mshambuliaji wa kati, na licha ya uwapo wa Kai Havertz, lakini bado kunaonekana kunahitaji la kumnunua mshambuliaji namba tisa.**

Kutumia fedha sasa ni jambo la lazima baada ya majeraha ya muda mrefu.

Hawa hapa ni washambuliaji sita ambao Arsenal wanaweza kujaribu kuwanunua Januari hii.

### Alexander Isak

Hakuna siri kuhusiana na Arsenal kutaka kumnunua mshambuliaji wa Newcastle United, Alexander Isak. Nyota huyo wa Sweden, ambaye amefananishwa na gwiji wa Washikabunduki hao, Thierry Henry, kwa muda mrefu amekuwa akipendekezwa kuhamia London Kaskazini, na kiwango chake cha kuvutia cha msimu huu wa 2024/25 kimeongeza mijadala kuhusu mustakabali wake.

Isak ametengeneza mabao 15 na asisti nne katika mechi 22 alizochezea 'Magpies' msimu huu huku akionekana kuongeza idadi yake ya mabao 27 pamoja kutoka msimu uliopita. Mshambuliaji huyo mwenye nguvu na kasi amefunga katika mechi zote mbili dhidi ya Arsenal msimu huu.

Kumsajili Isak hakutakuwa jambo rahisi. Newcastle inaripotiwa kuwa inamthaminisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kwa pauni milioni 150, ada ambayo itawakatisha tamaa wengi Ulaya. Januari inaweza kuonekana mapema sana kwa mabadiliko kama hayo, haswa na Arsenal katika nafasi dhaifu ya mazungumzo.

### Viktor Gyokeres

Raia mwingine wa Sweden ambaye Arsenal imekuwa ikivutiwa naye kwa muda mrefu ni Viktor Gyokeres, ambaye mwenyewe amefanikiwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani tangu ahamie Sporting CP mwaka 2023. Mshambuliaji huyo wa zamani wa Brighton & Hove Albion alifunga mabao 43 na kusaidia 14 kwenye mechi 50 alizocheza katika kampeni ya kwanza huko Lisbon.

Gyokeres anastaili, inayofanana na Isak kuhusiana na kasi yake na umbile. Bei inaweza isiwe juu sana lakini bado itafanya macho miamba hao wa Kaskazini mwa London kuwa na wakati mgumu, kwani anakadiriwa kuwa na thamani ya takriban pauni milioni 70 hadi 90 zinazohitajika kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ureno.

Huku Gyokeres akiwa bado hajajaribiwa kwenye Ligi Kuu England, ana umbile na ukatili unaohitajika kwa kikosi chochote kwenye kuzifumania nyavu. Mabao matano katika mechi sita za Ligi ya Mabingwa Ulaya - ikiwa ni pamoja na hat-trick dhidi ya Manchester City - inathibitisha uwezo wake.

### Benjamin Sesko

Tamaa ya Arsenal ya kuimarisha safu ya ushambuliaji si jambo geni. Benjamin Sesko aliripotiwa kuwa mlengwa mkuu wa klabu hiyo mwanzoni mwa msimu wa majira ya joto uliopita, lakini haraka akasaini mkataba wa nyongeza na RB Leipzig ambao ulifanya uhamisho wa kwenda Ligi Kuu England kutowezekana.

Akiwa na umri wa miaka 21 pekee, mshambuliaji huyo wa Slovenia bado hajaamuru mechi kwa njia sawa na wenzake, lakini ametoa namba thabiti mapema katika kazi yake. Alifunga mabao 18 akiwa na Leipzig msimu uliopita, hesabu ya kuheshimika.

Arsenal watakuwa wanalipa uwezo na Sesko taayari ni mshambulizi mzuri, lakini ana uwezo wa kuibuka namba tisa anayekipiga katika timu ya Emirates. Ada yake inatajwa kuwa kati ya pauni milioni 50 hadi 70 na inaweza kuwa kikwazo kwa Arsenal Januari hii.

### Santiago Gimenez

Ikiwa Kocha Mikel Arteta anataka mapendekezo kuhusu Santiago Gimenez, anahitaji tu kumpigia simu Kocha wa Liverpool, Arne Slot. Mholanzi huyo alisaidia kumlea mshambuliaji huyo wa Feyenoord walipokuwa pamoja huko Rotterdam, akiwa na mabao 49 katika misimu yake miwili iliyopita.

Mshambuliaji huyo wa kati mrefu na mwenye uwezo mkubwa wa kufunga ana umri wa miaka 23 tu, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Mexico ana muda mwingi wa kutatua matatizo yoyote.

Bila shaka, Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, ina rekodi mchanganyiko linapokuja suala la kuzalisha vipaji vya kiwango cha Ligi Kuu England, lakini Arsenal wanaweza kutuzwa haraka ikiwa watacheza kamari kwa Gimenez. Mshambuliaji huyo karibu ajiunge na Nottingham Forest msimu wa majira ya joto na huenda akawa mbadala wa bei nafuu kwa wengine kwenye orodha ya wanaotamaniwa na Washikabunduki hao.

### Liam Delap

Baada ya muda wa mkopo wa tatu na viwango tofauti vya mafanikio, Liam Delap hatimaye alifanikiwa kuhamia Ipswich Town kutoka Man City wakati wa majira ya kiangazi. Walimnunua kwa kitita cha pauni milioni 20 na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anaweza kuthibitisha mwokozi wao mwishoni mwa msimu.

Delap, mtoto wa mchezaji wa zamani wa Stoke City, Rory, ametengeneza mabao nane katika kipindi chake cha kwanza cha nusu msimu akiwa na Ipswich na amevutia macho kwa mbinu ya kushambulia. Ana uwezo mkubwa wa kuwapa wakati mgumu mabeki bora wa ligi.

Januari inaweza kuja mapema sana kwa Delap na Arsenal - ikiwa Washikabunduki hao wanavutiwa na kinda huyo, bila shaka - huku Ipswich ikiwa na uwezekano wa kuidhinisha kuondoka kwa hali yoyote. Bado, ni mmoja ambaye angeweka alama kwenye masanduku kadhaa kwa Washikabunduki.

### Jonathan David

Ni Robert Lewandowksi, Harry Kane na Erling Haaland pekee waliofunga mabao mengi katika ligi tano bora za Ulaya kuliko nyota wa Lille, Jonathan David mnamo 2024. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Canada alifikisha mabao 36 katika mwaka wa kalenda, idadi sawa na Kylian Mbappe na saba zaidi ya Mohamed Salah na Cole Palmer.

Sababu pekee ambayo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 anachukuliwa kuwa chaguo la 'gharama nafuu' Januari ni kutokana na ukweli kwamba mkataba wake unaisha msimu huu wa majira ya joto. Jambo kama hilo linaweza kuingia mikononi mwa Arsenal, huku Lille ikitarajiwa kukubali ofa ya takriban pauni milioni 20 hadi 25.

Ingawa Arsenal inaweza kusubiri na kumsajili David kwa msimu huu wa majira ya joto, kuweka fedha Januari itawaruhusu kushinda foleni na kuwapa mmoja wa washambuliaji wa kati bora zaidi Ulaya kwa kipindi cha pili cha msimu huku wakitarajia kumaliza ukame wao wa taji.

## Nukuu

"Unapoangalia uchezaji - sijui ni timu ngapi zinacheza katika kiwango hiki kama cha Liverpool kwenye ligi. Kiukweli nakionea wivu kikosi cha Liverpool ni kipana na imara sana, ukiangalia benchi lao, unaona kabisa tupo tofauti kabisa," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, baada ya juzi kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Aston Villa, huku Liverpool ikiisulubu Brentford 2-0.**



"Tulicheza na Man City na Arsenal na sasa Liverpool, kwa muda mfupi, Kwangu mimi [Liverpool] wako kiwango cha juu zaidi ya timu hizo mbili. Wamekamilika. Maadili yao ya kazi, jinsi wanavyorudi nyuma, ni viashiria vyema. Ni timu bora zaidi katika Ligi Kuu England na ulimwengu, wanapewa nafasi kubwa kushinda [taji]," **Kocha wa Brentford, Thomas Frank, baada ya kupoigwa mabao 2-0 dakika za majeruhi juzi. Hata hivyo Arsenal iliifunga 3-1 huku wakitoka sare ya 2-2 na Man City.**



"Nilisikia tayari nina mabao mengi zaidi yake hapa, kwa hivyo huo ni ushindi mmoja juu yake, niliifuata Newcastle nilipokuwa mdogo. Tunaweza kuwa na ndoto kubwa na kwenda mbali zaidi," **Mshambuliaji wa Bournemouth, Justin Kluivert ambaye juzi alifunga hat-trick, wakati wakishinda alivunja rekodi ya baba yake, Patrick Kluivert, ya kufunga mabao mengi (mawili zaidi) katika Uwanja wa St James' Park.**



# HIZI HAPA TAKWIMU 17 MECHI YANGA, MC ALGER




Straika wa Yanga, Clement Mzize, katika harakati za kutaka kumtoka kiungo, Reda Halaimia wa MC Alger ya Algeria, kwenye mchezo wa mwisho wa Kundi A, Ligi ya Mabingwa Afrika, uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na timu hizo kutoka suluhu. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara, Yanga, juzi walishindwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa kwa mara ya tatu mfululizo.

**Ni baada ya kulazimishwa suluhu dhidi ya MC Alger kutoka nchini Algeria na kuhitimisha safari yao msimu huu iliyoishia kwenye Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Msimu wa 2022/23, Yanga ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho na kuvuka hadi fainali, ikaukosa ubingwa kwa USMA Alger ya Algeria kwa tofauti ya bao la ugenini.

Ilifungwa mabao 2-1 nyumbani na kwenda kushinda bao 1-0 ugenini, hivyo matokeo ya jumla yakawa 2-2, Waalgeria wakanufaika na bao walilofunga, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Msimu uliopita ilifanikiwa pia kufika hatua ya robo fainali, Ligi ya Mabingwa Afrika na kutolewa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini kwa penalti 4-3, Aprili 5, mwaka jana, mechi iliyochezwa Sauzi, baada ya suluhu ya mechi zote mbili, ya kwanza ikichezwa Machi 30, mwaka jana, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Juzi, ilitaka kufanya hivyo kwa mara ya tatu kwenye mechi za kimataifa na mara ya pili, Ligi ya Mabingwa, ikihitaji ushindi wa aina yoyote, lakini ilishindwa kufanya hivyo mbele ya mashabiki wao, huku wapinzani wao wakihitaji ushindi au sare ambayo waliipata.

Matokeo hayo yameifanya MC Alger kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikifikisha pointi tisa, ikimaliza mechi sita za Kundi A, ikiwa nafasi ya pili na kuiacha Yanga ikimaliza nafasi ya tatu, ikiwa na pointi nane.

Vinara wa kundi hilo ambao walifuzu mapema ni Al Hilal Omduraman ya Sudan, iliyomaliza ikiwa na na pointi 10, juzi ikipokea kipigo cha mabao 4-0 dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, mechi iliyochezwa Uwanja wa Mazembe.

Katika makala haya, tunakuletea takwimu zote za mechi ya juzi, pamoja na msimamo wa kundi kwa mtindo wa namba, twende sasa...

**539#** Yanga ilipiga idadi hii ya pasi, zikiwa ni nyingi zaidi dhidi ya wapinzani wao katika mchezo wa juzi.

**260#** Hizi ni pasi zilizopigwa na wapinzani wa Yanga, MC Alger katika mchezo wa juzi uliomalizika kwa suluhu.

**84#** Ni pasi za Yanga zilizopigwa kwa usahihi zaidi katika mchezo wa raundi ya sita, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger, ikiwa pia imeongoza kwa kufanya hivyo.

**69#** Yanga ilimiliki mpira mara idadi hii katika mchezo wa juzi, ikiongoza kwa umiliki zaidi kuliko wapinzani wao.

**66#** Namba hii inasimama kama pasi za usahihi zilizopigwa na MC Alger katika mchezo huo wa mwisho wa Kundi A.

**31#** MC Alger ilimiliki mpira mara namba hii, ikiwa ni kiwango cha chini kuliko wenyeji wao Yanga, licha ya matokeo kuwa suluhu, kwani walionekana kucheza zaidi nyuma ya mpira.

**19#** Ni idadi ya faulo zilizopigwa na Yanga katika mchezo husika, ikiwa ni timu iliyopata faulo nyingi kuliko wapinzani wao.

**18#** Haya ndiyo mashuti ya jumla yaliyopigwa na Yanga katika mchezo wa juzi katika kile ambacho wachezaji wa timu hiyo walikuwa wakitafuta angalau bao moja ili kuweza kufuzu.

**14#** Hizi ni faulo ambazo MC Alger walifanikiwa kuzipata kwenye mchezo wa juzi, pungufu ya faulo sita ambazo wenyeji wao walizipata. Namba hii pia inasimama kama idadi ya kona ambazo Yanga imezipata katika mchezo huo.

**10#** Ni muda ambao mechi kati ya timu hizo mbili ulianza kwa saa za Afrika Mashariki na kumalizika saa 12 na ushehe hivi jioni.

**9#** Idadi ya pointi zilizoifanya MC Alger kushika nafasi ya pili na kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kutoka Kundi A.

**8#** Pointi ambazo Yanga imekusanya hadi mwisho wa mchezo wake wa Kundi A, ambazo bado hazikuiwezesha kutinga hatua ya robo fainali.

**6#** Idadi ya michezo ambayo timu zote zimecheza kwenye Kundi A, ambazo zimeziwezesha timu ya Al Hilal Omdurman ya Sudan na MC Alger kufuzu hatua ya robo fainali.

**3#** Yanga ilipiga idadi hii ya mashuti kwenye lango la wapinzani wao ambayo yalilenga lango. Pia ni idadi ya kadi za njano zilizotolewa kwenye mchezo wa juzi ambazo zote zilielekezwa kwa timu moja tu, MC Alger, huku Yanga ikiwa haijapata kadi yoyote. Namba hii pia inasimama kama ni idadi ya mashuti yaliyopigwa na MC Alger katika mchezo huo.

**2#** Timu zote mbili ziliotea mara idadi hii katika mchezo wa juzi, ambao hata hivyo, Yanga ndiyo ilitawala zaidi kuliko wapinzani wao ambao walitumia muda mwingi kukaa nyuma ya mpira na kushambulia kwa kushtukiza.

**1#** Ni idadi ya kona ambayo MC Alger ilipata, pamoja na shuti lao pekee lililolenga langoni kwa Yanga katika mchezo huo.

**0#** Hakukuwa na kadi ya njano wala nyekundu kwa Yanga, pia hakukuwa na kadi yoyote nyekundu kwa wageni MC Alger na hapakupatikana bao kwa timu yoyote.

**JE, WAJUA?**



MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Darwin Nunez, amehusika moja kwa moja katika mabao mengi kama mchezaji wa akiba kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye Ligi Kuu England tangu awasili klabuni hapo Juni 2022 (mechi 11, mabao saba, asisti nne), huku mabao nane kati ya 24 ya ligi ameyafunga katika dakika 15 za mwisho za michezo, kwa mujibu wa takwimu za ESPN.



## TAKUKURU yawapa maagizo walimu vita ya rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani Dodoma imewataka walimu kuweka jitihada za kuzisimamia klabu za wapinga rushwa zilizopo shuleni, ili kusaidia kuwajengea msingi bora wanafunzi wa kupambana na masuala ya rushwa.

Ofisa Uchunguzi Kiongozi Msaidizi kutoka TAKUKURU Dodoma, Faustine Malecha alisema hayo, wakati akitoa elimu kwa maofisa elimu ngazi ya Kata, Jiji pamoja na maofisa udhibiti ubora wa elimu katika mkutano uliohusisha kundi hilo uliolenga kuangalia mitaala mipya ya elimu iliotolewa na serikali.

Malecha, alisema klabu hizo zinapaswa kupewa ushirikiano pale wanapokuwa wanatoa elimu ya kupinga rushwa kwa wanafunzi wenzao ambao hawajajiunga katika klabu hizo ili nao wajiunge.

"Naomba sana mzipe ushirikiano klabu za wapinga rushwa zilizopo shuleni tunahitaji kuziona zinapiga hatua katika mapambano dhidi ya rushwa,"alisema Malecha.

Alisema, uanzishwaji wa klabu hizo shuleni katika shule mbalimbali ni moja ya njia ya kuwaandaa wanafunzi hao kuanzia ngazi ya chini kuwa mabalozi wazuri wa kupinga rushwa hapo baadae.

Mbali na hilo aliwasisitiza maofisa elimu kata na wakuu wa shule kuwa mstari wa mbele katika suala zima la kupiga vita rushwa, huku akiwasisitiza kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa katika maeneo mbalimbali.

Mwelimisha Umma kutoka TAKUKURU Dodoma, Idda Siriwa aliwataka maofisa hao, kuwa makini na vitendo vya rushwa kwa sababu vinachangia kuharibu ikiwemo kurudisha nyuma maendeleo ya taifa.

Alisema jamii hususani kundi hilo la maofisa elimu kuanzia ngazi ya Kata, Jiji pamoja na maofisa udhibiti ubora wa elimu mkoani Dodoma kuwa mstari wa mbele kukemea vitendo vya rushwa na siyo kuvikumbatia.

"Tunaomba zingatieni hii elimu ya kuzuia rushwa itawasaidia kulinda heshima na utu wenu kwenye utumishi wa umma, mkifanya hivyo hamtakumbana na rungu ya rushwa,"alisema Siriwa.

# RC atangaza msako kaya zisizokuwa na vyoo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ametangaza kuanza kwa operesheni ya kuzisaka kaya zisizokuwa na vyoo na kuwachukulia hatua, ili kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambao umekuwa ukitokea mara kwa mara mkoani hapa.

Akizungumza juzi katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), alisema ni aibu kila mara mkoa kukumbwa na mlipuko wa kipindupindu kutokana na sababu kadhaa ikiwamo ukosefu wa vyoo kwa baadhi ya watu jambo ambalo serikali haitakubali kuona likiendelea.

"Kuanzia kikao hiki operesheni ya kuwasaka watu wasiokuwa na vyoo ianze mara moja kabla ya mvua hazijaanza kuwa nyingi na watakaobainika hawana vyoo hatua kali zichukuliwe," alisema.

**Kuhusu suala la lishe, Dendego aliwataka madiwani na wabunge suala la lishe kwa watoto liwe kipaumbele kuelimisha wananchi na kuhakikisha wanafunzi**

Kuhusu suala la lishe, Dendego aliwataka madiwani na wabunge suala la lishe kwa watoto liwe kipaumbele kuelimisha wananchi na kuhakikisha wanafunzi wote wanapata chakula wanapokuwa shuleni.

Awali Mganga Mkuu wa Mkoa wa Singida, Victorina Ludovick, akiwasilisha hali ya afya katika kikao hicho alisema changamoto kubwa iliyopo katika mkoa ni kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.

Alisema katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Desemba 2024 mlipuko wa kipindupindu uliripotiwa katika halmashuri za Wilaya ya Manyoni, Iramba na Ikungi na kusababisha vifo vya watu saba.

Ludovick alisena hadi kufikia Desemba 31, 2024 watu waliougua ugonjwa huo walikuwa 464 ambapo kati ya hao 253 wakitoka Halmashuri ya Wilaya ya Manyoni, 184 Halmashuri ya Wilaya ya Ikungi na 27 katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba.

Kuhusu vyoo alisema kaya ambazo hazina vyoo kabisa ni asilimia 2.2, zenye vyoo bora ni asilimia 75.5 na wenye vyoo vya asili ni asilimia 24.9.



Ofisa Elimu Maalumu wa Jiji la Dodoma, Issa Kambi akimwangalia mtoto mwenye ulemavu na mahitaji maalumu kwa ajili ya usahili wa kumwandikisha shule ya watoto wenye ulemavu, katika Kata ya Chang'ombe, jijini humo juzi. Kushoto ni mama wa mtoto huyo, Mwajuma Hassani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Halmashauri zaagizwa kutenga bajeti uchimbaji visima

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule ameziagiza halmashauri zote mkoani hapa kutenga bajeti ya kuchimba visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali.

Pia, amewataka maofisa ugani kutumia ujuzi wao kuwaelimisha wakulima katika maeneo mbalimbali mkoani hapa ili wafanye kilimo cha kitaalamu ambacho kitawapa matokeo chanya.

Senyamule, alisema hayo juzi jijini hapa alipofanya ziara ya kutembelea shamba darasa la Jeshi la Magereza lililopo Makao Makuu ya Jeshi hilo Msalato jijini hapa.

Alisema kila halmashauri mkoani hapa, inapaswa kutenga bajeti ya kuchimba kisima ambacho kitawasaidia wakulima kufanya kilimo chenye tija, kitawasaidia kupiga hatua na kuondokana na kilimo cha mazoea.

"Halmashauri mnapaswa kutenga bajeti ya kuchimba visima kwa ajili ya wananchi kuendesha kilimo cha umwagiliaji, serikali imewekeza kwenye sekta ya kilimo, hivyo jitahidi kuwasaidia wakulima kwenye ubunifu wa miundombinu ya uwagiliaji," alisema Senyamule.

Alisema ili wakulima wapige hatua katika kilimo wanahitaji elimu ya kitaalamu kutoka kutoka kwa maofisa ugani ili waweze kuondokana na kilimo cha mazoea na kujikita katika kilimo cha kisasa cha umwagiliaji.

Kadhalika, alisema maofisa ugani wanapaswa kutumia ujuzi wao kuwaelimisha wakulima katika maeneo mbalimbali kuhusu kilimo cha kisasa ili kujikwamua kiuchumi.

Kuhusu shamba darasa la Jeshi la Magereza, Senyamule alisema wakulima wanapaswa kwenda kujifunza kilimo cha kitaalamu kinachofanywa kupitia wataalamu wa kilimo ili kuongeza ujuzi ikiwemo kwenda kubadilisha kilimo wanachofanya.

Senyamule alisema kutokana na umahiri walionao Jeshi la Magereza kwenye sekta ya kilimo anaamini ushirikiano wao baina ya wakulima utazidi kushawishi wakulima kufanya kilimo cha kitaalamu ambacho kitawadaidia kuongeza uzalishaji katika mazao mbalimbali.

# Samia mgeni rasmi mkutano mkuu ALAT

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), utakaofanyika Februari mwaka huu jijini Mwanza.

Mwenyekiti wa ALAT, Taifa Murshid Ngeze, alibainisha hayo juzi jijini hapa, wakati akifungua kikao cha kamati tendaji kwa ajili ya kujadili ajenda mbalimbali ikiwemo mkutano mkuu wa mwaka wa jumuiya hiyo.

Ngeze, alisema mkutano huo ambao ni wa mwisho kwenye uongozi wao umepangwa kufanyika jijini Mwanza mwezi ujao ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Nigusie kuhusu mkutano wetu wa mwisho katika uongozi wetu ambao tulimwalika Rais Samia kuwa mgeni rasmi hapa nimwagize katibu kuhakikisha kuwa mambo yote yanayohusu mkutano huu yanakuwa sawa ili tumwandikie barua ya kumkumbusha kwa ajili ya kuwa mgeni rasmi" alisema

Aidha, alisema ili kufanyikisha mkutano huo mshikamano ndani ya jumuiya hiyo ni muhimu kwakuwa hakuna taasisi ambayo inaweza kuendelea bila kuwa na umoja.

"Nipongeze kwa mshikamo uliopo baini yetu naomba uendelee taasisi yoyote ili iendele lazima muwe na mshikamo bila mshikamno hatuwezi kwenda mbele nawashukuru sana kwa namna ilivyo sasa," alisema.

Vile vile, alisema ili kuimarisha uhusiano wa nadi na nje ya jumuiya hiyo katibu anapaswa kuandika baruka katika nchi mbili ambazo kamati tendaji ianweza kujigawa kwa ajili ya kufanya ziara ya kwenda kuimarisha mahusiano.

"Katibu andika nchi mbili ambazo kamati inaweza kujigawa ikaenda kutembelea na kumarisha uhusiano hata kama haitafanyika hivi sasa wakati wa uongozi wetu lakini mapendekezo yawepo kwa ajili ya kwenda kuimarisha mahusiano" alisema.

Naye Katibu Mkuu wa ALAT, Mohammed Maje, alisema katika kupanua wigo wa uhusiano wanatarajia kukutanao na mabalozi mbalimbali nchini ikiwemo wa Denmark, Sweden na Marekani.

Kadhalika, alisema tayari wamepeleka taarifa za kueleza kuwa Jumiya ya ALAT ni nini, lakini pia kuwaeleza uhusiano na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Hata hivyo, alisema ajenda za kiako hicho ni pamoja na kufungua kikao, kuthibitisha ajenda, kusoma na kuthibitisha muktasari wa kikao kilichopita, kusoma mapato na matumizi, taarifa ya utekelezaji wa shughuli za ALAT pamoja na mengineyo.



# Watatu mbaroni tuhuma za kuwauzia wakulima mbegu feki

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe kwa kushirikiana na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) limewakamata watu watatu kwa tuhuma za kuuza mbegu feki katika Kijiji cha Kidugala kilichopo wilayani Wanging'ombe mkoani Njombe.

Hayo yalielezwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki.

Alisema mbegu zilizokamatwa ni aina ya tembo yenye kilo 286 ambazo zilikuwa zikiuzwa kwa wakulima wakiambiwa ni mbegu za tembo wakati siyo kweli.

Alisema wananchi wa Njombe wamekuwa na uhitaji wa mbegu, hivyo matapeli kwa kulijua hilo wanatumia mbinu mbalimbali ili kuwatapeli wakulima na kujipatia fedha zisizo halali.

"Wameshawazia watu wengi mpaka sisi tunakuja kupata taarifa na kushirikiana na watu wa TOSCI na kuna baadhi walipanda mbegu zile hazikuweza kuota," alisema Banga.

Alisema idadi halisi ya watu waliouziwa mbegu hizo feki haijafahamika kwakuwa wapo wanaotoa taarifa na wengine hawatoi ila waliofika kituo cha polisi na kuandika maelezo walikuwa wakulima sita.

Alisema jeshi hilo litakapokamilisha uchunguzi wake watuhumiwa hao wote watatu watafikishwa mahakamani ili kujibu mashtaka ambayo yanawakabili ya kuuza mbegu feki za mahindi.

**Alisema jeshi hilo litakapokamilisha uchunguzi wake watuhumiwa hao wote watatu watafikishwa mahakamani ili kujibu mashtaka ambayo yanawakabili ya kuuza mbegu feki za mahindi.**

Mmoja wa wauzaji na msambazaji wa pembejeo za kilimo mkoani Njombe, Frank Luoga alisema uhaba wa mbegu na mbolea ndiyo unaosababisha wakulima kuuziwa mbegu au mbolea feki.

"Mfano mbegu sasa hivi toka msimu wa kilimo uanze wakulima wanahangaika sana mbegu hakuna sasa wakati huo wanawapa mianya wahalifu waweze kufanya hivyo," alisema Luoga.

Hivyo, aliiomba serikali kuhakikisha kuwa pembejeo za kilimo zinapatikana kwa wakati na kuwafikia wakulima hiyo itapunguza mianya ya watu kutengeneza mbegu na mbolea ambazo hazifai.

Wakati huo huo, jeshi hilo limemkamata Brujo Mapunda mkazi wa Iringa kwa kosa la kuingilia kwenye mfumo kinyume cha sheria na kufanikisha kuiba Sh. milioni 19.8 kutoka kwenye akaunti ya CRDB ya mfanyabiashara kutoka Kijiji cha Usuka wilayani Wanging'ombe.

Alisema: "Kuna utapeli ambao unaendelea watu wanafika kwa watu na kusema wanapandisha 4G wananchi wetu wamekuwa na tabia ya kuwapatia simu na kuwaruhusu kupandisha hiyo 4G lakini watu hawa wamekuwa wajanja wanachunguza kwenye simu wanakuta kuna akaunti na kwa bahati mbaya kuna watu wanaweka password zao kwenye namba za simu yule anazi-



Watendaji wa uboreshaji ngazi ya Mkoa wa Mtwara, wakishiriki katika mafunzo ya vitendo ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, jana, zoezi linalotarajiwa kufanyika mkoani humo, kuanzia Januari 28,2025 hadi Februari 03, 2025 katika maeneo yote ya mkoa huo, Mkoa wa Lindi pamoja na Halmashauri za Madaba, Namtumbo na Tunduru kwa Mkoa wa Ruvuma. **PICHA: INEC**

# Somo la utunzaji mazingira laanza kufundishwa 'chekechea'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WIZARA ya Elimu imeanza kufundisha somo la utunzaji wa mazingira kuanzia darasa la awali ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki katika mafunzo kwa walimu wanaofundisha darasa la awali na walimu wakuu wa shule za msingi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako yaliyofanyika mjini humo.

Akizungumza na walimu hao, mwenzeshaji wa mafunzo hayo kitaifa, Jerome Mwakifuna alisema kutokana na uwepo wa mitaala mipya ya elimu, serikali imeanza kufundisha somo la utunzaji wa mazingira kwa wanafunzi wa awali ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema masomo mengine ambayo yatatolewa kwa wanafunzi wa awali ni pamoja na somo la sayansi, hisabati pamoja na somo la lugha ya Kiswahili.

"Mitaala hii mipya inaenda kumfundisha mtoto kwa vitendo zaidi hali itakayomsadia kujitegemea kwani ni muda mzuri wa kumjengea msingi mzuri mtoto ni pale anapokuwa chini ya miaka minane," alisema Mwakifuna.

Naye Ofisa Elimu Taaluma Halmashauri ya Mji wa Makambako, Shaban Ambwindile aliwataka wazazi kukubaliana na mabadiliko hayo ya mitaala ya elimu na kueleza kuwa endapo watoto wataanza kujengewa msingi mzuri wakiwa wadogo itakuwa ni rahisi kwao kufikia ndoto zao.

"Wazazi wakubaliane na mabadiliko lakini pili wawe karibu na watoto kwa sababu watoto wanajengewa na wazazi, walimu pamoja na mazingira yanayowazunguka," alisema Ambwindile.

Kwa upande wake, Ofisa Elimu Awali na Msingi Halmashauri ya Mji wa Makambako, Samweli Komba aliwataka walimu ambao wamepata mafunzo hayo kuhakikisha wanayafanyia kazi ili watoto wapate elimu sahihi.

"Kama mnavyojua tunaendana na mabadiliko ya kisera, sayansi na teknolojia hivyo watoto hawa wapate dozi ya kwenda kupambana na kujua wapo katika dunia gani," alisema Komba.

Baadhi ya walimu akiwemo Furaha Mgeni alisema watahakikisha wanafanyia kazi mafunzo hayo na kueleza kuwa mitaala mipya itasaidia kwa kiasi kikubwa watoto kujitegemea huku akiomba wazazi kushirikiana nao ili kukuza taaluma na malezi ya watoto.

# DC awapa nasaha wanufaika mikopo asilimia 10

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe mkoani Njombe, Kissa Kasongwa amewataka wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 kuhakikisha wanatumia fedha hizo kwa kufanya shughuli walizokusudia ili waweze kurejesha na siyo vinginevyo.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akikabidhi hundi ya mikopo ya asilimia 10 yenye thamani ya shilingili milioni 474.95 kwenye vikundi 81 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika Halmashauri ya Mji wa Makambako.

Alisema kuwa kama fedha hizo zitatumika tofauti itasababisha kushindwa kuzirejesha na hivyo kusababisha wengine kushindwa kukopa.

"Nendeni mkatumie fedha hizi kwa malengo mliokusudia, lakini mkifanya vinginevyo mtashindwa kurejesha na wengine watashindwa kukopa naomba mzingatie sana hili," alisema Kissa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hanana Mfikwa aliwataka wanufaika wa mkopo huo kutotumia fedha hizo kwenye sherehe mbalimbali na kueleza kuwa sharti la mkopo wowote ni kuamka mapema na kufanya kazi kwa bidii ili kupata faida na marejesho.

Naye Katibu wa Mbunge wa Jimbo la Makambako, Vasco Mgunda aliwataka wanufaika wa mikopo hiyo kuhakikisha fedha hizo haziwi chanzo cha migogoro kwenye ndoa zao.

Nao wanufaika wa mkopo huo akiwemo, Prosper Vedasto alisema watahakikisha wanatumia kwenye miradi itakayo waingizia kipato ili wazijerejeshe kwa wakati.

Katika mikopo hiyo, vikundi 57 vya wanawake vimekopeshwa kiasi cha shilingi milioni 352.6, vikundi 14 vya vijana mililioni 86.25 na watu wenye ulemavu 10 wakikopeshwa kiasi cha shilingi milioni 36.1.



# Uchaguzi Mkuu watibua tamasha la utalii, uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema maonesho ya pili ya utalii na uwekezaji Zanzibar yanatarajiwa kufanyika Mei mwaka huu badala ya Oktoba, ili kupisha shughuli za Uchaguzi Mkuu.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maonesho hayo, Waziri Soraga alisema kutokana na mafanikio ya maonesho ya kwanza yalilofanyika Oktoba mwaka jana wameamua kwa mwaka huu yafanyike Mei ili kupisha shughuli za Uchaguzi Mkuu.

Alisema sekta ya utalii ipo imara na katika kuelekea Uchaguzi Mkuu, ni wakati wa kuzidi kujenga imani kwa wawekezaji na wageni kwa sababu mara nyingi uchaguzi huwa unayumbisha sekta ya utalii na uwekezaji.

Kadhalika, alisema Zanzibar kwa kiasi kikubwa ilikuwa washiriki wa matukio kama hayo ya utalii yaayofanyika maeneo mbalimbali, lakini wanakosa kutangaza bidhaa za utalii zilizopo Zanzibar na ndio maana wakamua kuazisha maonesho hayo ili kuwaleta watu mbalimbali duniani kufika Zanzibar na kujionea kilichopo.

Alisema wanatarajia maonesho hayo kuwa na washiriki zaidi ya 1,000 na kutanua wigo wa matukio ambayo yatafanyika ikiwemo mafunzo ya uwekezaji wa wadau wa utalii.

Alisema rekodi zinaonesha kuwa katika kipindi cha Desemba mwaka jana Zanzibar imepokea watalii wengi zaidi na kuvunja rekodi kwa kupokea watalii zaidi ya 90,000 kwa mwezi mmoja.

Alisema Zanzibar imeshapata tuzo ya maeneo muhimu la matukio ya utalii, hivyo ni muhimu kuendeleza kushajihisha kuwa na matukio mengi zaidi watalii kufika kwa wengi na kujionea ubora wa visiwa hivyo.

Alisema sekta ya utalii ni muhimu kwa sababu inachangia zaidi ya asilimia 30 ya pato la taifa na zaidi ya asilimia 80 ya fedha za kigeni, hivyo kila mmoja anawajibu kuendelea kuwa imara na kushamiri kwa sekta hiyo.

Hata hivyo alisema lazima uwekezaji na utalii uzingatie uhifadhi na uendelevu wa mazingira ili kisiwa hicho kuendelea kutunzwa maana kadri wageni wanavyokuwa wengi ndivyo inaweka mkazo zaidi katika suala la uhifadhi wa mazingira.

# Zanzibar yatangaza bei mpya ya umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), imepandisha bei ya umeme kwa wateja wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi ya umeme visiwani hapa.

Imesema kuongezeka kwa mahitaji hayo kumesababisha uhitaji wa kuwapo maboresho ya lazima ya miundombinu ya umeme, ili kukidhi mahitaji.

Akitangaza mabadiliko ya bei hiyo kwa waandishi wa habari visiwani hapa, Meneja Uhusiano ZURA, Mbarak Hassan Haji, alisema bei mpya za umeme zitaanza kutumika leo.

Alisema uniti moja kwa wateja wa majumbani wenye matumizi madogo ya wastani wa uniti 50 kwa mwezi waliounganishwa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V) watauziwa kwa Sh.84 badala ya Sh. 79 ikiwa ni ongezeko la shilingi tano.

Mbarak alisema wateja wa umeme wamegawika katika makundi manne ambao ni majumbani wenye matumizi madogo ya wastani wa yuniti 50 kwa mwezi waliounganishwa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230v) na wateja wenye matumizi ya kawaida hususani wateja wa majumbani, wenye biashara ndogo, maduka waliounganishwa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V) na njia tatu (400V).

> **"Kwa wateja waliounganishwa katika msongo mkubwa wa umeme ambao hao ni wafanyabiashara wenye viwanda vya kati na vikubwa kwa sasa watauziwa umeme uniti moja kwa Sh. 178 badala ya Sh.169,"**

Aliwataja wateja wengine ni waliounganishwa katika msongo mdogo na msongo wa kati wa umeme ambao hao ni wafanyabiashara wenye viwanda vidogo pamoja na wateja waliounganishwa katika msongo mkubwa wa umeme ambao hao ni wafanyabiashara wenye viwanda vikubwa.

Aidha, alisema wateja wenye matumizi ya kawaida hususani wateja wa majumbani, wenye biashara ndogo, maduka waliounganishwa katika msongo mdogo wa umeme kwenye njia moja (230V) na njia tatu (400V) kwa sasa watanunua umeme uniti moja kwa Sh. 310 badala ya Sh. 288.

Kuhusu bei mpya kwa wateja waliounganishwa katika msongo mdogo na msongo wa kati wa umeme ambao hao ni wafanyabiashara wenye viwanda vidogo, alisema kwa sasa watanunua umeme uniti moja kwa Sh. 217 badala ya Sh. 206.

"Kwa wateja waliounganishwa katika msongo mkubwa wa umeme ambao hao ni wafanyabiashara wenye viwanda vya kati na vikubwa kwa sasa watauziwa umeme uniti moja kwa Sh. 178 badala ya Sh.169," alisema Mbarak.

Pia alisema bei hizo zimetoa punguzo la Sh. 190 kwa watumiaji wadogo ambao walikuwa wakilipa Sh. 480 kwa uniti kila wanapovuka matumizi ya uniti 50 kwa mwezi ambapo sasa watalipa Sh. 290 kwa uniti moja.

Hata hivyo alisema mabadiliko hayo hayatahusisha tozo ya kutoa huduma na bei ya mahitaji ya juu zitabaki kama zilivyo.

Alisema umeme uliopo ambapo Zanzibar inapokea umeme kutoka Tanzania Bara unatosheleza ingawa serikali inampango wa kuongeza nishati mbadala ya umeme ukiwemo wa jua na upepo.

Alisema changamoto iliyopo njia zinapokea umeme zimezidiwa kutokana na watumiaji umeme kuongezeka na kutatua changamoto hiyo serikali inajenga miundombinu mengine ya njia za kupitisha umeme.




Meneja wa kitengo cha uhusiano wa Mamlaka ya udhibiti wa maji na nishati Zanzibar (ZURA), Mbarak Hassan Haji akizungumza na waandishi wa habari, Maisara Zanzibar jana, wakati akitangaza bei mpya ya umeme Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watumishi ZRA watakiwa kuzingatia sheria, kanuni

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), wametakiwa kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa umma katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mkurugenzi Utafiti na Mipango kutoka ZRA, Ahmed Haji Saadat, aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya uadilifu katika ukusanyaji wa mapato kwa wafanyakazi na watendaji wa Mkoa wa Kaskazini kikodi katika ofisi za ZRA Kiwengwa.

Alisema ni lazima wafanyakazi kuzifahamu na kuzijua sheria zote, kanuni na taratibu zilizokuwepo nchini ili kujiepusha na makosa katika utumishi wa umma.

Aidha, alisema hawawezi kufanya kazi kama kanuni hawajui na ndiyo nguzo ya kujenga maadili katika utendaji wao wa kila siku katika utumishi.

Pia, aliwasisitiza kuzingatia na kuyaishi maadili katika utendaji wao na kuimarisha hali ya uadilifu katika utumishi wao ili ZRA iwe taasisi yenye kufanya kazi vizuri katika jambo hilo.

Alisema ofisi za mikoa za ukusanyaji wa mapato zina umuhimu mkubwa katika kukusanya kodi, kutoa huduma na kusimamia maadili.

Naye Mkuu wa kitengo cha kusimamia maadili ya wafanyakazi, Khamis Ramadhan Khamis, alisema mafunzo hayo yana umuhimu mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Alisema lazima ifahamike kuwa maadili siyo wizi pekee bali jambo hilo linaingia kwenye nidhamu, uadilifu, kuheshimu viongozi na wafanyakazi lakini pia wafanyabiashara ambao ndiyo walipakodi wao.

Alisema ZRA ina mkakati wa kupambana na rushwa na eneo hilo lina chukua nafasi kubwa katika maadili ya watendaji ambao wanakusanya kodi na wapo hatarini.

Alisema ZRA imeunda kamati ya usimamizi wa maadili na tayari imeshaanza kufanya kazi, hivyo aliwasisitiza wafanyakazi kuwa makini katika utekelezaji wa majukumu yao kwa kufanya kazi kwa nidhamu, uadilifu na uwajibikaji.

Kamanda Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) mkoa huo, Ali Seif Ali, alisema lengo mafunzo hayo ni kuzifikia taasisi zote kuzipatia elimu kwasababu mamlaka hiyo imeundwa kwa malengo makuu matatu ikiwemo kufanya uchuguzi, kutoa elimu kwa umma juu ya elimu ya rushwa na kufanya udhibiti.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**PAULINA CHRISTOPHER** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0960-0196** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BENJAMIN W. MKAPA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/6059/2025.**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**JOAVIN HUSSEIN HOBA** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye **NO.TAE3371265** kuanzia tarehe 24 MARCH 2020 na kuisha muda wake tarehe 23 MARCH 2030. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/3476/2025.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN SOLOMON MADAHA** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index **No S.0172/0026** Mwaka 2018 Shule ya Sekondari **DON BOSCO SEMINARYI,** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa . Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **PHQ/DOD/DOD/2632/2025.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU Mkoa wa SIMIYU**

**Shauri la Madai/Ndoa Na.01/2025**

**Jina la Mdai: HULDA NKONYA**

**Jina la Mdaiwa: SABATO SUSU**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa SABATO SUSU**
**WA NYANGUGANWA**
**MASWA.**

**K.K M/KITONGOJI**
**NYANGUGANWA**

**KK: WEO**
**SHANWA, MASWAI.**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao (Eleza hapa habari za Madai)Ameleta madai kuwa **ANADAI TALAKA ILI MUACHANE.**
Kwa hiyo unatakuwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 01 Mwaka 2025. saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hatohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini ,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 15 Mwezi 01 Mwaka 2025.

**Hakimu**
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU**

MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU MASWA

HAKIMU MKUU MAHAKAMA YA MWANZO NYALIKUNGU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**

**Kituo cha BUGANDO Mkoa GEITA**

**Shauri a madai/Ndoa Na 01/2025**

**Jina la Mdai: THOMAS BONIPHACE**

**Jina la Mdaiwa: SHABAN ABDALAH**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:SHABAN ABDALAH**
**WA KIJIJI CHA SENGA GEITA**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba Unaamriwa na Jamhuri uhudhurie Mahakamani hapa ili ujibu madai ya fedha,2,800,000/- za mdai Thomas Boniphace
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 21 Mwezi 01 Mwaka 2025 saa 3.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea. ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 09 Mwezi 01 Mwaka 2025

FAHAMU

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO BUGANDO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo Cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 02/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMIS JUMA SAID WA CHANG'OMBE KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SALAMA MOHAMED ABED**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 7 Mwezi 2 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
* Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 3 Mwezi 01 Mwaka 2025

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI DODOMA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF RUNGWE**
**AT TUKUYU**

**CIVIL APPEAL CASE NO: 24460 OF 2024**

**GOODLUCK SANGA...........................APPELLANT**

**VERSUS**

**BEMENYIMANA PIERRE CELESTIN............RESPONDENT**

**TO: BENYIMANA PIERRE CELESTIN**

**TAKE NOTICE** that the hearing of the above appeal has been set down for MENTION on 20 day of 1, 2025 at 08:30 AM.

You must produce on that day all witnesses upon whose evidence and all the documents which you intend to rely in support of your case.

**GIVEN UNDER MY HAND AND SEAL OF THIS COURT** this 8 day of 1, 2025.

GIVEN UNDE.

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
RUNGWE/TUKUYU.

Place: RUNGWE/TUKUYU
Copy to: ...

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 521 YA MWAKA 2025.**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**STEVEN SHADRACK KANGERO**

**NA**

**MKUNDE STEVEN KANGERO...................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyoye kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 4 mwezi Machi, 2025. Saa 12.00 Mchana. Siku ambayo Shauri hili limepangwa kusikilizwa Mbele Mhe.Jaji S.D MWAIPOPO.
Imesainiwa Dar es Salaam, leo tarehe 17 mwezi Januari, 2025.

HIGH COURT OF TANZANIA

NAIBU MSAJILI

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 521 OF 2025**

**In the Matter of the Estate of the Late STEVEN SHADRACK KANGERO**

**In the Matter of an Application for Letters of Administration**

**BY**

**MKUNDE STEVEN KANGERO.................... PETITIONER.**

**TO: STEVEN JUNIOR MAXWELL**
**SPAIN**

**SUMMONS TO APPEAR**

You are hereby summoned to appear in this court on 4TH March, 2025. 12:00 a.m before **Hon. S.D. MWAIPOPO, JUDGE**
GIVEN under my hand and Seal of the Court this 17TH January, 2025

HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 521 OF 2025**

**In the Matter of the Estate of the Late STEVEN SHADRACK KANGERO**

**In the Matter of an Application for Letters of Administration**

**BY**

**MKUNDE STEVEN KANGERO...................... PETITIONER.**

**TO: SHADRACK FRANKLIN KANGERO**
**DAR ES SALAAM**

**SUMMONS TO APPEAR**

You are hereby summoned to appear in this court on 4TH March, 2025. 12:00 a.m before **Hon. S.D. MWAIPOPO, JUDGE**
GIVEN under my hand and Seal of the Court this 17TH January, 2025

HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 521 OF 2025**

**In the Matter of the Estate of the Late STEVEN SHADRACK KANGERO**

**In the Matter of an Application for Letters of Administration**

**BY**

**MKUNDE STEVEN KANGERO...................... PETITIONER.**

**TO: JOYCE STEVEN KANGERO**
**UNITED STATES OF AMERICA,**
**4610 GREENWOOD STREET,**
**LINCOLN NEBRASKA 68504 USA.**

**SUMMONS TO APPEAR**

You are hereby summoned to appear in this court on 4TH March, 2025. 12:00 a.m before **Hon. S.D. MWAIPOPO, JUDGE**
GIVEN under my hand and Seal of the Court this 17TH January, 2025

HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 521 OF 2025**

**In the Matter of the Estate of the Late STEVEN SHADRACK KANGERO**

**In the Matter of an Application for Letters of Administration**

**BY**

**MKUNDE STEVEN KANGERO.....................PETITIONER**

**TO: FAITH SHADRACK KANGERO**
**AUSTRALIA**

**SUMMONS TO APPEAR**

You are hereby summoned to appear in this court on 4TH March, 2025. 12:00 a.m before **Hon. S.D. MWAIPOPO, JUDGE**
GIVEN under my hand and Seal of the Court this 17TH January, 2025

DEPUTY REGISTRAR

HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 521 OF 2025**

**In the Matter of the Estate of the Late STEVEN SHADRACK KANGERO**

**In the Matter of an Application for Letters of Administration**

**BY**

**MKUNDE STEVEN KANGERO.....................PETITIONER.**

**TO: MOHAMED STEVEN S. KANGERO @MOHAMED STEVEN KANGERO@ SANTOS STEVEN S. KANGERO UNITED STATES OF AMERICA**

**SUMMONS TO APPEAR**

You are hereby summoned to appear in this court on 4TH March, 2025. 12:00 a.m before **Hon. S.D. MWAIPOPO, JUDGE**
GIVEN under my hand and Seal of the Court this 17TH January, 2025

HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TEMEKE HIGH COURT SUB – REGISTRY**
**(ONE STOP JUDICIAL CENTRE)**
**AT TEMEKE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 521 OF 2025**

**In the Matter of the Estate of the Late STEVEN SHADRACK KANGERO**

**In the Matter of an Application for Letters of Administration**

**BY**

**MKUNDE STEVEN KANGERO..................PETITIONER.**

**TO: DAGLESS SHADRACK KANGERO**
**DUBAI, UAE**

**SUMMONS TO APPEAR**

You are hereby summoned to appear in this court on 4TH March, 2025. 12:00 a.m before Hon. S.D. MWAIPOPO, JUDGE
GIVEN under my hand and Seal of the Court this 17TH January, 2025

HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR

---

**FORM NO 02B**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**

**MAHALI: KIGOMA**

**MAOMBI NA 66 MWAKA 2023**

**KAGIMBO HOSEA ALPHONCE.........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**MTAWA HAMIS MABIRU NA ALLY RAMADHANI**

**MJIBU MAOMBI..................................WANYAMA**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: MTAWA HAMIS MABIRU NA ALLY RAMADHANI@WANYAMA POPOTE MLIPO**

Fahamu kwamba shauri hii limepangwa kutajwa tarehe 23 Mwezi 01 Mwaka 2025 saa 2:30 Asubuhi mbele ya Mheshimiwa F. CHIMIKU Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 18 Mwezi 12 Mwaka 2024

MWENYEKITI

---

**FORM NO 02B**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**

**MAHALI: KIGOMA**

**MAOMBI NA 43 MWAKA 2023**

**MGENI RASHIDI MGENI (MSIMAMIZI WA MIRATHI) YA MWOMBAJI**

**MAREHEMU RASHIDI MGENI LWEMERA**

**DHIDI YA**

**RAMADHANI RASHIDI OKALA................MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: RAMADHANI RASHIDI OKALA POPOTE ULIPO**

Fahamu kwamba shauri hii limepangwa kutajwa tarehe 23 Mwezi 01 Mwaka 2025 saa 2:30 Asubuhi mbele ya Mheshimiwa F. CHIMIKU Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 18 Mwezi 12 Mwaka 2024

MWENYEKITI

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED NASSOR ALLY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 320 ABV** aina ya HINO. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/IRI/IRI/1041/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RABANI PETRO SAIMON** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 470 DLP – KINGLION** yenye jina la umiliki wa **JOHNMMADUKA COMPANY LIMITED.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBE/2575/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**PILLY HAMISI MSUMI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 901 AAT – TVS KING.** Chassis namba **MD6M14PK8E4A29657.** Engine namba **OK4AE1035324.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/14379/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GIDEON MATUMA ZEPHANIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye majina THOMAS ANYITIKE MWAMMALE namba za usajili **T 857 BND** aina ya **Toyota RAV 4 ,** Chassis No. **AC21015612,** Engine No. **1AZ4150878.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/CHE/55896/2024**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Maelfu waandamana Trump akikaribia kuapishwa leo

**WASHINGTON,** Marekani

MAELFU ya wananchi wengi wao wakiwa wanawake wameandamana mjini Washington Marekani wakilalamika dhidi ya kuapishwa kwa rais mteule Donald Trump, huku wakitoa ujumbe wa kulindwa kwa haki zote za kiraia na kibinadamu.

Rais mteule wa Marekani Trump anatarajiwa kuapishwa mapema leo ili kurejea tena katika Ikulu ya White House kuliongoza taifa hilo, baada ya kumshinda mpinzani wake Makamu wa Rais Kamala Harris katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi Novemba mwaka jana.

Ilielezwa kuwa wananchi hao walijitokeza barabarani jana kuanzia uwanja wa Franklin na kupita kati kati ya jiji la Washington hadi uwanja mkubwa mbele ya makumbusho ya Lincoln.

Ilielezwa kuwa waandamanaji walikusanyika pamoja na kusikiliza hotuba kutoka kwa viongozi wa asasi mbalimbali za kiraia kuhusiana na kulinda demokrasia, haki za wanawake ikiwemo za uzazi, na usawa wa kijinsia.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Popular Democracy, Analilia Mejia alisema maandamano hayo yana lengo la kuwaleta pamoja wanaharakati na waungaji mkono ili kuwakumbusha masuala muhimu ya demokrasia yanayokabiliwa na kitisho chini ya utawala mpya.

Anasema ujumbe muhimu ni kuhakikisha vita vinaendelea na mageuzi ya kweli yanapatikana baada ya vita vya muda mrefu.

Ilielezwa kuwa maandamano ya mwaka huu ya kupinga kuapishwa kwa Trump yamekua madogo zaidi kuliko yale yaliyofanyika wakati wa awamu yake ya kwanza 2017.

Pia ilielezwa kuwa vuguvugu la kutetea haki za wanawake Marekani limegawika baada ya Trump kumshinda makamu wa rais Kamala Harris mwezi Novemba. **VOA**




Maandamano ya wananchi wa Marekani yalipoanza kutoka uwanja wa Farragut, Washington, wakidai haki ya wanawake kuelekea kuapishwa kwa rais mteule Donald Trump, jana. **PICHA: MTANDAO**

## DRC kuchunguza ubadhirifu wa madini

**KINSHASA,** DRC

WIZARA ya Sheria nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imesema serikali imeanzisha uchunguzi kuhusu ubadhirifu wa zaidi ya dola milioni 300 kutoka kwa mchimbaji madini wa serikali kampuni ya Gecamines wakati ikiendesha shughuli hiyo kati ya 2012 na 2020.

Inaelezwa kuwa kampuni ya Gecamines, ambayo ina hisa chache katika miradi mikubwa zaidi ya shaba na kobalti duniani, imekuwa ikitawaliwa na shutuma za ufisadi zinazotolewa na mashirika yasiyo ya kiserikali na wanasiasa wa upinzani.

Ilibainishwa kuwa Shirika la uangalizi wa fedha za umma la DRC, ambalo linafanya Ukaguzi Mkuu wa Fedha (IGF), liligundua mwaka 2022 kwamba zaidi ya dola milioni 400 za malipo ya kodi na mikopo ambayo Gecamines ilisema ililipa kwa hazina ya kitaifa haikupatikana.

Ilisema katika ripoti ya wakati huo kwamba dola milioni 413 zilizopotea zilidhaniwa kuwa zilifujwa na kwamba wakaguzi wa hesabu wataendelea na uchunguzi wao.

Hata hivyo, Gecamines ilikanusha mara kwa mara kufanya makosa, huku IGF ikieleza kuwa iligundua katika ukaguzi tofauti wa fedha za benki kuu ya DRC kwamba Gecamines ilikuwa imefuja malipo ya kodi ya awali yenye thamani ya karibu dola milioni 315 kati ya 2012 na 2020.

Wizara ya sheria ya DRC ilisema imemwagiza mwendesha mashtaka wa umma kufungua kesi mahakamani dhidi ya wale waliohusika na ufujaji wa fedha za umma uliotiwa alama na IGF.

Ilisema kutakuwa na mkazo mahususi katika ubadhirifu wa malipo ya kodi ya mapema yenye thamani ya takriban dola milioni 315 kati ya 2012 na 2020. **TRT**

# 10 wauawa Gaza licha ya mkataba wa usitishaji vita

**GAZA,** Palestina

TAKRIBAN Wapalestina 10 wameuawa na 25 kujeruhiwa katika mashambulio ya Israel huko ukanda wa Gaza ikiwa ni zaidi ya saa moja kupita tangu makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya Israel na Hamas yalipotarajiwa kuanza kutekelezwa.

Kwa mujibu wa maofisa wa hospitali na ulinzi wa raia katika Ukanda wa Gaza mauaji hayo yalitokea asubuhi ya jana, wakati hali ya sintofahamu ikitanda juu ya hatima ya makubaliano hayo huku mashambulizi ya anga ya Israel yakiendelea huko Gaza.

Msemaji wa ulinzi wa raia wa Gaza Mahmoud Basal alisema "Milipuko wa mabomu bado inaendelea katika maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Gaza, hasa mji wa Gaza na kaskazini".

Maofisa hao walieleza kuwa mashambulizi hayo yalisababisha vifo vya watu sita katika kitongoji cha Al-Shaaf mashariki mwa Jiji la Gaza, watatu kaskazini mwa mji wa Gaza, pamoja na mmoja katika mji wa kusini wa Rafah.

Shambulio hilo la mabomu limekuja baada ya makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyokuwa yakitarajiwa kucheleweshwa huku Israel ikisisitiza kwamba haitasonga mbele hadi Hamas itakapotoa majina ya mateka watakaoachiliwa.

Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu alisema usitishaji wa mapigano hautaanza hadi Hamas itakapotoa orodha ya mateka watakaoachiliwa. Huku Hamas ikalaumu juu ya kucheleweshwa kwa usitishaji vita.

Saa chache baada ya kauli ya waziri huyo Kundi la Hamas lilitoa ujumbe kwenye Telegram kwamba imetoa majina ya mateka watatu wa kike ambao inasema itawaachilia kwanza, kama sehemu ya usitishaji vita na Israel, hatua iliyoifanya ofisi ya Waziri Mkuu Netanyahu kusema usitiswaji utaanza muda wowote.

Katika hatua nyingine, Chama cha siasa kali za mrengo wa kulia cha Jewish Power kimesema kinaacha madaraka ndani ya serikali ya Israel kwa kupinga makubaliano ya kusitisha mapigano, na kumwacha Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu akiwa amesalia na wabunge wachache.

Ilielezwa kuwa Waziri wa usalama wa taifa hilo Itamar Ben-Gvir, pamoja na Yitzhak Wasserlauf na Amichai Eliyahu, wamewasilisha barua zao za kujiuzulu jana asubuhi.

Kadhalika, ilielezwa kuwa Ben-Gvir kwa muda mrefu amekuwa mpinzani mkubwa wa makubaliano ya kusitisha mapigano, na ameshinikiza Israel kuendelea na operesheni yake ya kijeshi dhidi ya Hamas huko Gaza.

Akimwandikia Netanyahu kutangaza kujiuzulu, Ben-Gvir alisema hatafanya kazi ya kupindua serikali, lakini akataja makubaliano ya kusitisha mapigano kuwa ushindi kamili kwa ugaidi.

Hata hivyo, kwa mujibu wa CNN vikosi vya Israel vimeonekana kuondoka kutoka sehemu za kati na mashariki mwa mji wa Rafah huku Gaza.

Vile vile, ilielezwa kuwa baadhi ya Wapalestina wameanza kurejea katika miji iliyokumbwa na vita kaskazini mwa Gaza, ikiwa ni pamoja na Beit Hanoun na kambi ya wakimbizi ya Jabalya. **CNN, BBC**

# COASTAL YATANGAZA KUINGIZA WACHEZAJI TISA DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union, imetangaza kusajili jumla ya wachezaji tisa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili lililofungwa Januari 15, mwaka huu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema jana kuwa wachezaji hao wamesajiliwa kutokana na mapendekezo ya Kocha Mkuu, Juma Mwambusi, ambaye ametaka kuongezewa nguvu kwenye kikosi hicho.

"Tumesajili wachezaji tisa, tunatarajia watakuja kutupa kile ambacho tunakitarajia, tunawasubiri kwa hamu kubwa uwanjani. Tunawakaribisha sana kwenye klabu hii kongwe katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, yenye mashabiki wenye upendo wa hali ya juu," alisema Sabri.

Wachezaji ambao Coastal Union imewaongeza kipindi cha uhamisho wa dirisha dogo la usajili lililofungwa usiku wa Jumatano kuamkia Alhamisi iliyopita, ni Rafael Daud Lothi kutoka Singida Black Stars, Rithie Nkoli aliyesajiliwa akitokea Namungo FC, pamoja na mwenzake Moza Kristom Abdallah. Wengine ni Mgaza Hamisi Ally, aliyetoka kucheza soka la kulipwa Falme za Kiarabu, Aron Ally Kalambo (Geita Gold), Sabri Kondo, Fales Gama Andrea wakisajiliwa kutoka Klabu ya Yanga kwa vijana chini ya miaka 20, Gustaph Somon (Dodoma Jiji) na Enrick Vitalis Mkosi wa Fountan Gate.

Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, Coastal Union imeshika nafasi ya 11 kwenye msimamo, ikiwa na pointi 18 kwa michezo 16 iliyocheza mpaka sasa.

Timu hiyo, imeshinda michezo minne, sare sita na kupoteza mechi sita, ikifunga mabao 16 na kuruhusu wavu wake kuguswa mara 17.

Msimu uliopita, timu hiyo ilimaliza ligi ikiwa nafasi ya nne, na kufanikiwa kucheza mechi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Bravos do Maquis ya Angola, ikitolewa kwa jumla ya mabao 3-0, ikifungwa idadi hiyo ya mabao ugenini na kulazimishwa suluhu nyumbani.



Straika wa Yanga, Prince Dube, akipasua katikati ya mabeki wa MC Alger ya Algeria, kwenye mchezo wa mwisho wa Kundi A, Ligi ya Mabingwa Afrika, uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa sare tasa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *KenGold yavunja rekodi usajili madirisha yote*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KenGold imevunja rekodi ya usajili kwenye kipindi cha dirisha dogo kilichomalizika Jumatano iliyopita, kwa kusajili wachezaji wengi zaidi kuliko timu yoyote ile kwenye Ligi Kuu.

Timu hiyo imetia fora kwa kusajili jumla ya wachezaji 22, idadi ambayo ni kubwa zaidi hata kwenye usajili wa dirisha kubwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, jana, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Jose Mkoko, amesema wamefanya usajili kutokana na mapendekezo ya kitaalamu, hasa baada ya kuona kikosi chao kimekuwa dhaifu kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

"Ni kweli, tumesajili wachezaji wengi, lakini ni mapendekezo yaliyotolewa na wataalam, nadhani tulikosea mwanzo, lakini hatutaki kukosea tena. Hatutaki kuendelea kubaki mkiani kwenye mechi za mzunguko wa pili," alisema Mkoko.

Wachezaji waliosajiliwa na timu hiyo kuelekea kwenye mzunguko wa pili, ni Bernard Morrison, Obrey Chirwa, Erick Kabamba, Fredrick Kalubunga kutoka Vipers ya Uganda, Kelvin Yondani, kiungo wa zamani wa Yanga, Zawadi Mauya, Emmanuel Asante kutoka Namungo, Mubashid Seidu kutoka nchini Ghana, Kyala Lassa, akisajiliwa kutoka nchini Zambia na Ernest Kwofie akitokea Ghana.

Wengine ni Thompson Unachi aliyesajiliwa kutoka nchini, Nigeria, Mohamed Yusuph kutoka Dodoma Jiji, Mathias Juviliani, Nassir Bofu, Abdul Abdulai, Maulid Mbegu, Sele Bwenzi, Joseph Ambokege, Ahmed Chambela, Sadala Lipangile, Sandale Komanje na Rogars Gabriel.

Hadi mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu unamalizika, KenGold imeambulia pointi sita tu kwa michezo 16 iliyocheza, ikiburuza mkia, ikishinda mchezo mmoja tu, sare tatu, ikipoteza michezo 12.

# Singida BS kupiga mechi 2 za kirafiki

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Singida Black Stars kinatarajiwa kucheza michezo miwili ya kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara itakayoanza mapema Februari mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Hussein Masanza, alisema mpaka sasa wapo kwenye mchakato wa kutafuta timu ambazo watacheza nazo.

"Tunatarajia kucheza michezo miwili ya kirafiki tukipata timu ambazo tutacheza nazo tutawapa taarifa ili Watanzania wafahamu tunacheza na nani, alisema," Masanza.

Alisema timu yao kwa sasa inaendelea na mazoezi ili kuhakikisha inaendeleza ushindani katika michezo yao itakayocheza mzunguko wa pili.

Masanza (pichani) alisema wachezaji waliowasajili kipindi cha usajili wa dirisha dogo wataongeza ushindani katika kikosi chao na kwamba wamechukua nyota wenye viwango vya kimataifa.



"Wachezaji ambao tumewasajili ninaamini wataleta ushindani katika timu yetu kwani lengo letu ni kushiriki mashindano ya kimataifa," alisema.

Aliwataka mashabiki wao kuendelea kuwaunga mkono wachezaji wao hao kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani pindi ligi hiyo itakaporea.

Wakati huo huo, timu Ken Gold nayo inatarajiwa kucheza mchezo wa kirafiki Jumatano wiki hii dhidi ya Tanzania Prison ikiwa ni maandalizi kuelekea michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ifikapo mwezi ujao.

Mchezo huo utapigwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Jose Mkoko alisema kikosi kinaendelea na mazoezi na kwamba baadhi ya wachezaji waliowasajili wanatarajiwa kuwasili kambini leo, Jumatatu.

"Wachezaji wetu Zawaidi Mauya, Ronas Gabriel pamoja na Selemani Bwenzi bado hawajaripoti kambini, tunawatarajia kesho (leo) kuungana na wenzao kambini ili kuendelea na mazoezi ya pamoja," alisema Mkoko.

## ZISIKUPITE

### WAKOMAA NA SESKO

ARSENAL inapanga kuweka dau la pauni milioni 70 kumnunua mshambuliaji wa RB Leipzig, Benjamin Sesko, 21, kwenye dirisha la uhamisho la mwezi huu, au kujadiliana kwa mkopo wa muda mfupi. ***(The Sun)***

### DELE KUSAINI COMO

WINGA wa zamani wa England, Dele Alli, 28, anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa kuichezea Klabu ya Como iliyopo Serie A inayonolewa na Cesc Fabregas. ***(Fabrizio Romano)***

### WALKER KUTUA MILAN

ZLATAN Ibrahimovic, ambaye ni mshauri mwandamizi wa wamiliki wa AC Milan, amethibitisha nia ya klabu hiyo kutaka kumsajili beki wa kulia wa Manchester City, Kyle Walker, 34. ***(Mail, via DAZN)***

### CAMBIASO HANA OFA

MKURUGENZI wa Michezo wa Juventus, Cristiano Giuntoli, amesema klabu hiyo ya Italia haijapokea ofa kutoka Manchester City ya kumtaka beki wao, Andrea Cambiaso, 24. (***Goal, via DAZN***)

### MENDEZ KUBAKI PSG

MLINZI wa kushoto wa Ureno, Nuno Mendes, 22, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, huenda akabakia na Paris St-Germain. ***(L'Equipe)***

### AIT-NOURI AFIKIRIA

MANCHESTER United pia inamfikiria beki wa Wolves na Algeria, Rayan Ait-Nouri, 23. ***(Independent)***

### FERGUSON ASUBIRIWA RASMI

WEST Ham na Bournemouth ni miongoni mwa klabu zinazosubiri habari kuhusu iwapo mshambuliaji wa Brighton, Evan Ferguson, 20, atapatikana kwa mkopo mwezi huu. ***(Express)***

### SILVA ANAFUATILIWA WOLVES

KIUNGO wa kati, Manu Silva, 23, aliyeachwa nje ya kikosi cha Vitoria kwa mchezo wao wa Jumamosi - anafuatiliwa na Wolves. ***(Wolverhampton Express & Star)***

### CORNET ANUKIA GENOA

GENOA ya Italia imefanya makubaliano ya kumsajili Maxwel Cornet, 28, ambaye amekuwa kwa mkopo Southampton kutoka West Ham. ***(Fabrizio Romano)***

### AWINDWA ARSENAL

ARSENAL, Chelsea na Bayern Munich ni miongoni mwa klabu zinazotaka kumsajili beki wa kati wa Sporting, Ousmane Diomande, 21. ***(Caught Offside)***

### YAIKATALIA CHELSEA

DEPORTIVO La Coruna huenda ikalazimika kumuuza winga, Yeremay Hernandez, 22, ingawa Deportivo inasemekana imekataa ofa ya awali ya Chelsea kwa vile wanataka kiasi cha pauni milioni 17. ***(Caught Offside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: NINAPATA WIVU MKUBWA KWA LIVERPOOL

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekiri kuwa na wivu mkubwa kwa kikosi cha Liverpool baada ya Arsenal kupoteza nafasi kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England kwa sare ya mabao 2-2 dhidi Aston Villa, Jumamosi.

**Saa chache baada ya Liverpool kufunga mabao mawili dakika za lala salama na kuifunga Brentford 2-0, Arsenal walisalimu amri kwa sare kwenye Uwanja wa Emirates na kuachwa pointi sita na vinara hao ambao wana mechi moja mkononi.**

Mabao ya Gabriel Martinelli na Kai Havertz yaliiweka Arsenal kwenye nafasi ya kupata pointi zote tatu, kabla ya mabao mawili ndani ya dakika nane kutoka kwa Youri Tielemans na Ollie Watkins kuwafanya wagawane ponti moja-moja na Villa.

> Ukiangalia benchi lao, unaona kabisa tupo tofauti kabisa, kiukweli nakionea...

Wakati kocha wa Liverpool Arne Slot alimtumia mshambuliaji wa pauni milioni 85, Darwin Nunez kutoka benchi ambaye alifunga mabao mawili ya dakika za lala salama.

"Kuna nyakati katika mbio za ubingwa zinakuwa wazi. Liverpool walikuwa na faida ya kuwa na kikosi kipana na kufanikiwa kubadili mchezo. Kwa upande wetu, ilikuwa kinyume chake," alisema Arteta.

"Ghafla timu ilipata gia nyingine ya kwenda tena na kuwaweka Aston Villa kwenye boksi lao na kwenda na kwenda tena na kujaribu kutafuta bao ambalo hawakuweza kufunga."

Arsenal wanajaribu kuongeza angalau mchezaji mmoja kabla ya dirisha la usajili la Januari hii kufungwa kwa muda wa wiki mbili zilizobaki.

Alipoulizwa kama anaweza kuifikia Liverpool kwenye mbio za ubingwa, Arteta alijibu: "Unapoangalia uchezaji - sijui ni timu ngapi zinacheza katika kiwango hiki kama cha Liverpool kwenye ligi.

"Kiukweli nakionea wivu kikosi cha Liverpool ni kipana na imara sana. Ukiangalia benchi lao, unaona kabisa tupo tofauti kabisa."

HABARI MICHEZO

# SLOT: NUNEZ ANAJIWEKEA REKODI LIVER



**LONDON,** England

ARNE Slot amesema ustadi wa Darwin Nunez wa kufunga mabao muhimu ya dakika za mwisho kwa Liverpool ni "nzuri kuwa nao" baada ya mshambuliaji huyo kufanya hivyo tena na kuipa timu yake ushindi muhimu dhidi ya Brentford Jumamosi.

Nunez alifunga mabao mawili katika muda wa nyongeza na kupata ushindi wa 2-0 wa Liverpool katika mchezo ambao ulikuwa na wastani wa mashuti 48 golini.

Kwa mujibu wa takwimu za ESPN, Nunez amehusika moja kwa moja katika mabao mengi kama mchezaji wa akiba kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye Ligi Kuu England tangu awasili Juni 2022 (mechi 11 mabao saba, asisti nne), wakati mabao nane kati ya 24 ya ligi ameyafunga katika dakika 15 za mwisho za michezo.

"Siku zote huwa na mchango mkubwa anapoingia," alisema Slot akiiambia BBC.

"Yeye huleta nguvu na hapo ndipo yuko katika ubora wake.

"Saa ya kwanza mara nyingi huwa wazi, lakini dakika 30 za mwisho zinatawala. Kisha kuwa na mtu kama Darwin ni vizuri sana.

"Siangalii matokeo tu, tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini sasa ni ushindi kwa hiyo sipaswi kusema kuangalia utendaji wetu. Nilifurahishwa sana na wachezaji wetu, kwani Brentford walipigana na wapo vizuri."

Ushindi huo huko London Magharibi ulikuwa wa kwanza kwa Liverpool katika ligi tangu mwanzoni mwa mwaka huu na ulimaliza kuyumba kwa timu ya Slot baada ya sare na Manchester United na Nottingham Forest na kufungwa na Tottenham Hotspur kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Carabao.

Slot alikiri kwamba hakuwa na uhakika kwamba kikosi chake kingepata njia ya kushinda mchezo huo huko London Magharibi.

"Nilikuwa na shaka juu ya hilo kwa sababu kabla hatujafunga mabao hayo mawili, nilihisi kana kwamba nilikuwa nikitazama mchezo mmoja tena na tena na tena kwa mtindo uleule," alisema Slot.

"Kwa hiyo nilisema tayari mara chache katika mahojiano mengine kwamba dhidi ya United, kila mtu alizingatia nafasi ya Maguire, lakini dakika saba kabla tulipata nafasi tatu za wazi.

"Kwa hiyo, mara nyingi sana katika wiki za hivi karibuni dhidi ya Tottenham pia - tulikosa nafasi nyingi. Dhidi ya Forest vile vile, tulikosa mengi. Kwa hiyo ndio, ingekuwa ya kushangaza kama tusingeshinda."

# Davies aota mbawa Real

**MADRID,** Hispania

ALPHONSO Davies anayelengwa na Real Madrid anakaribia kufikia makubaliano na Bayern Munich kuhusu mkataba mpya, kwa mujibu wa ripoti.

Davies ameingia miezi sita ya mwisho ya mkataba wake wa sasa na alikuwa akitarajiwa kwa muda mrefu kuondoka kwa uhamisho wa bure msimu ujao wa majira ya joto, huku Madrid wakionekana kuwa ndio wenye nafasi ya kumsajili.

Mapema wiki hii, ilionekana kwamba Davies alikuwa amechukua hatua nyingine karibu na mlango wa kutokea huku wakala wake akiondoka Munich bila makubaliano ya maslahi mapya.

Liverpool, Manchester City na Manchester United zote zilitarajiwa kuwasilisha ofa ya kumsajili kwa uhamisho wa bure.

Na sasa gazeti la The Athletic limefichua kwamba Davies anakaribia kuweka kalamu kwenye mkataba mpya na Bayern.

Makubaliano bado hayajafikiwa, lakini Bayern na Davies sasa wanaaminika kukaribia kufikia muafaka na kumaliza sintofahamu iliyodumu kwa muda mrefu kuhusu mustakabali wa beki huyo wa kushoto.

Hili linaweza kuwa pigo kubwa kwa Madrid kwani Sky Sports ya Ujerumani iliripoti hivi majuzi kwamba Davies alikuwa sehemu ya mpango pamoja na kiungo Jamal Musiala, huku wachezaji wote wakiweka wazi kuwa wanataka kuendelea kucheza pamoja.

Mkataba mpya wa Davies, utasaidia matumaini ya Bayern kumfunga Musiala kwenye mkataba mpya.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani, anayelengwa na Madrid na Manchester City, amebakiwa na miezi 18 kukamilisha makubaliano yake ya sasa.




# *Fati kuondoka Barcelona Januari hii*

**BARCELONA,** Hispania

ANSU Fati anatarajiwa kuondoka Barcelona kabla ya mwisho wa dirisha la uhamisho la Januari hii kufungwa baada ya kushindwa tena kujumuishwa kwenye kikosi cha Kocha Hansi Flick katika mecho dhidi ya Getafe, Jumamosi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, ambaye anaripotiwa kulipwa takriban pauni 200,000 kwa wiki, amekosa sehemu kubwa ya msimu huu kutokana na majeraha, lakini hajawa sehemu ya kikosi cha Flick cha LaLiga tangu aliporejea.

Fati aliingia akitokea benchi katika ushindi wa Copa del Rey dhidi ya Barbastro, lakini ameachwa nje ya kila kikosi cha siku ya mechi tangu wakati huo.

Fati alisafiri na kikosi hadi Saudi Arabia kwenye Supercopa de Espana, lakini aliachwa nje kwenye mchezo wa nusu fainali na fainali.

Kisha alitazama ushindi wa Copa del Rey dhidi ya Real Betis kutoka nyumbani na hakusafiri pia kukabiliana na Getafe.

Gazeti la Sport limeandika kuwa Barcelona imekubali kumuachia Fati, ambaye alikaa kwa mkopo katika Klabu ya Brighton & Hove Albion msimu uliopita.

Na sasa klabu hiyo ya Katalunya inatafuta sehemu mpya ya kucheza kwa winga huyo.

Klabu za Ligi Kuu England, Tottenham Hotspur na West Ham United zimeonesha nia ya kutaka kumsajili Fati, ambaye pia anavutiwa na Real Betis, Sevilla na timu ya Serie A, Como, inayonolewa na kiungo wa zamani wa Barcelona, Cesc Fabregas.

Mkopo unaonekana kuwa ndio matokeo yanayotarajiwa zaidi, huku Barcelona wakijiandaa kwa hitaji la kugharamia sehemu kubwa ya mshahara wa Fati, lakini uhamisho wa kudumu pia ni pendekezo lao.

## Ramovic: Ushindi kirahisi Ligi Kuu

INATOKA UK. 24

vizuri na imewalipa, huku akisema nguvu na hasira zao sasa wanazielekeza kwenye Ligi Kuu na Kombe la FA.

"Tulifanya kila tunachoweza kukifanya, lakini jamaa walikuwa imara sana, hawakuja Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya kitu chochote kile zaidi ya kutafuta sare na wameipata, soka limeamua matokeo.

"Tumepoteza, tunakwenda kujipanga, tutarudi tukiwa imara zaidi. Hasira zetu sasa tunarudi kwenye ligi ili kutetee makombe yetu, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA," alisema Kamwe.

Matokeo hayo, yameifanya MC Alger kufuzu hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ikifikisha pointi tisa, ikimaliza mechi sita za Kundi A, ikiwa nafasi ya pili na kuiacha Yanga ikimaliza nafasi ya tatu, ikiwa na pointi nane.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa MC Alger, Khaled Benyahia, alisema amefurahi kuingia hatua ya robo fainali licha ya kuwa mchezo haukuwa rahisi.

"Tumefurahi kwani malengo yetu yalikuwa ni kuingia hatua ya robo fainali ya mashindano haya, kwa sasa tunakwenda kujipanga kwa ajili ya michezo ijayo," alisema Benyahia.

Alisema Yanga ni timu nzuri yenye wachezaji wengi wenye uzoefu, hivyo waliingia wakiwa na tahadhari ya kutowaruhusu kupata bao.

Wakati huo huo Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma, alisema kutolewa kwa Yanga kunawafanya kwenda kufanya vzuri kwenye michezo ya Ligi Kuu.

"Yanga kutolewa hapa nafahamu watajipanga waweze kufanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu, hicho ni kitu cha kawaida kwenye mpira, kuna kufunga, kufungwa na kutoka sare, alisema Mwinjuma.

## Simba baba lao

INATOKA UK. 24

dakika ya 61, kwa shuti kali nje ya eneo la hatari, baada ya wachezaji wa Simba kufanya msako mkali, Elie Mpanzu akamweka mfungaji ambaye alipiga shuti la kushtukiza lililomwacha kipa Bouhalfaya akiruka bila mafanikio.

Wenyeji walizidisha mashambulizi na kufanikiwa kupachika bao la pili lililotiwa ndani ya kamba na Ateba.

Kipa Camara aliuanzisha kwa Fondoh Che Malone, ambaye aliukokota kwa umbali mrefu kwenye wingi ya kulia, kabla ya kumpa Kapombe aliyekuwa ameingia ndani kidogo, ambaye alipiga nusu krosi, iliyomkuta mfungaji akiwa katikati ya mabeki wawili na kipa wao. Aliwazidi nguvu na ujanja kabla ya kuujaza wavuni.

Kwa matokeo hayo, Simba ambayo inasubiri droo ya michuano hiyo ili kujua itacheza na nani, itaanzisha ugenini na kumalizia nyumbani kitu ambacho wanachama, mashabiki, viongozi na Kocha Mkuu, Fadlu Davids walikuwa wanakihitaji.

# KIPA YANGA ATUA SINGIDA BS, POKOU AKITABIRIWA MAKUBWA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Singida Black Stars, amemtabiria makubwa winga wake mpya, Serge Pokou, aliyesajiliwa kutoka Al Hilal Omdurman ya Sudan, huku ikikiri kumpokea kipa, Amas Obasogie raia wa Nigeria kutoka Yanga kwa makubaliano maalum.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Hussein Masanza, amesema kuwa usajili wa Pokou, umeonekana kuwashtua mashabiki wengi wa soka nchini kwani alikuwa akitakiwa na klabu kubwa za Simba na Yanga, lakini wao wamefanikiwa kumtwaa, akisema ni mchezaji atakayetikisa ligi ya Tanzania.

"Tunajua kuwa ni mchezaji mzuri ambaye klabu kubwa za Simba, Yanga zilikuwa zinamtaka, si mgeni machoni mwa mashabiki wa soka, kwani ameshawahi kuzifunga timu hizo, kwa maana hiyo tunajua anayajua mazingira yote ya hapa nchini, angalia tulivyomtambulisha nchi yote ilitetemeka, ni usajili wa 'sapraizi' kwa wengi.

"Tunaamini si mchezaji wa kusubiri muda, kama alipokuwa akitua tu na Al Hilal anafanya balaa, basi balaa kubwa zaidi linakuja," alisema Masanza.

Pokou, raia wa Ivory Coast, alifunga bao katika mchezo wa kirafiki mwaka jana Simba ikicheza dhidi ya Al Hilal katika mchezo wa kirafiki uliochezwa, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, zikitoka sare ya bao 1-1, pia aliwahi kuifunga Yanga kwenye mechi za Ligi ya Mabingwa misimu miwili iliyopita.


**Mbali na mchezaji huyo, Masanza amesema wameingia makubaliano maalum na Yanga, kumchukua kipa wao, Obasogie, raia wa Nigeria.**

"Kipa huyo amesajiliwa na Yanga, lakini tumemchukua kwa makubaliano maalum, haya ni masuala ya kawaida kwenye mpira wa miguu hivyo si ajabu sana," alisema.

Awali, kipa huyo alikuwa akiichezea Fasil Kenema FC ya Ethiopia, ambapo pia mara kwa mara amekuwa akiitwa kuunda kikosi cha Timu ya Taifa ya Nigeria.

Ofisa Habari huyo, ametangaza kuwasajili straika raia wa Ghana, Jonathn Sowar na Eliuter Mpepo, huku ikiachana na Joseph Guede ambaye amemaliza mkataba wake na klabu hiyo.

## KICHWA KWA MGUU...



Kiungo wa Aston Villa, Youri Tielemans, akicheza mpira kwa kichwa huku kiungo wa Arsenal, Mikel Merino, akitia mguu wakati wakiwania mpira kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Emirates na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# *Metacha, Chalamanda watisha uokoaji penalti*

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya magolikipa watano wa Ligi Kuu Bara, wameokoa mikwaju ya penalti hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa jana na Bodi ya Ligi, makipa hao kila mmoja ameokoa penalti moja. Hakuna kipa yeyote aliyeokoa zaidi ya penalti moja, huku wengine wakifungwa na baadhi timu zao hazijaruhusu adhabu hiyo kubwa kwenye lango lao.

Makipa waliocheza penalti mpaka sasa ni Metcha Mnata wa Singida Black Stars na Hussein Masalanga, ambaye amerejea Klabu ya Singida Black Stars, baada ya kucheza kwa mkopo Tabora United. Hata hivyo penalti aliyookoa ilikuwa kwenye kikosi cha Tabora United.

Wengine ni Jonathan Nahimana wa Namungo FC, Ley Matampi wa Coastal Union ambaye kwa sasa amevunja mkataba na klabu hiyo, baada ya dirisha dogo la uhamisho lilipofunguliwa Desemba 15, mwaka jana na Ramadhani Chalamanda wa Kagera Sugar.

Takwimu hizo za Bodi ya Ligi, zimeitaja Simba kuwa ndiyo timu iliyopata penalti nyingi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

Timu hiyo imepata penalti sita mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo la Nipashe ni kwamba, Simba imefunga penalti zake zote, kupitia kwa Jean Ahoua na Leonel Ateba, kila mmoja akifunga tatu.

Timu za Coastal Union, Namungo na Tabora United kila moja imebahatika kupata penalti tano, huku Azam FC, Fountain Gate na Yanga zikipata penalti tatu kila moja.

# Michezo



Jumatatu Januari 20, 2025

Nipashe

Davies aota mbawa Real Madrid UKURASA 22

# Simba baba lao CAF

## Kibu, Ateba waipeleka kileleni Kundi A wakiisambaratisha CS Constantine kwa...

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya kipindi cha pili, yaliyofungwa na Kibu Denis na Leonel Ateba, jana kwenye Uwanja wa Banjamin Mkapa, Dar es salaam, yaliiwezesha Simba kuondoka na ushindi wa 2-0 dhidi ya CS Constantine ya Algeria na kuongoza Kundi A la Kombe la Shirikisho Afrika.

**Ateba raia wa Cameroon, aliweka rekodi ya kufunga bao moja katika mechi mbili mfululizo, kwani katika mchezo uliopita dhidi ya Bravos do Maquis, uliochezwa nchini Angola, Januari 12, mwaka huu, alipachika bao la kusawazisha, lililoiwezesha Simba kutoka sare ya bao 1-1 na kufuzu hatua ya robo fainali.**

Ushindi huo umeiwezesha Simba kumaliza mechi zake sita za kundi hilo ikiwa kinara kwa kufikisha pointi 13, ikishinda michezo minne, sare moja, ikipoteza mmoja, ikifunga mabao manane na kufungwa manne.

Kipigo hicho kimeifanya CS Constantine kumaliza nafasi ya pili, ikikusanya pointi 12 nyuma ya Simba, ambapo katika michezo yake sita, imeshinda minne, imepoteza miwili na haijatoa sare yoyote.Katika mechi ya jana timu zote mbili zilikuwa tayari zimefuzu, badala yake zilikuwa zinatafuta kinara wa kundi.

Iwapo wachezaji wake wangekuwa makini, Simba ingeweza kuondoka na idadi kubwa ya mabao kutokana na kupata nafasi nyingi ambazo walishindwa kuzitumia.

Mechi ilianza taratibu, Simba wakimiliki kwa kiasi kikubwa huku wapinzani wao wakijazana nyuma kwani walihitaji sare tu ili kuweza kuongoza kundi.

Kutokana na hali hiyo, wachezaji wa Simba walikuwa wakipigiana pasi fupi fupi, kati na pembeni kwa lengo la kutaka kuwavuta CS Constantine, lakini walionekana wako makini katika mpango mkakati wao huo.

Kukosekana kwa nafasi kulimfanya Jean Ahoua kuamua kuachia shuti kali la mbali dakika ya 12, lakini mpira ukapaa juu ya lango.

Kiungo mshambuliaji huyo alipata nafasi nzuri dakika nne baadaye kutoka kwa Mpanzu, akiwa anatazamana na kipa, lakini alipiga shuti kali akiwa karibu na lango lililopanguliwa na mlinda mlango Zacharia Bouhalfaya.

Ahoua alishindwa kuitendea haki faulo aliyofanyiwa Kibu Denis dakika ya 21, badala yake akapaisha mpira juu.

CS Constantine ilifanya shambulio kwa mara ya kwanza kwenye lango la Simba dakika ya 25, ambalo lilikuwa la hatari, kwani Brahim Dib, aliwatoroka mabeki na kubaki na kipa, Moussa Camara, lakini wakati ameinua mguu wake wa kushoto kutaka kuukwamisha wavuni, Shomari Kapombe alimuwahi na kuutoa nje, ikawa kona.

Dakika ya 29, nahodha Mohamed Hussein 'Tshabalala' alitaka kufanya kile alichokifanya kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa nchini Algeria, Desemba 8, mwaka jana, alipopiga krosi iliyokwenda moja kwa moja hadi wavuni, lakini jana mpira wake uligonga mwamba wa juu na kutoka nje.

Ahoua aliikosesha Simba bao dakika ya 37, baada ya kazi kubwa ya Ateba kuwatoka mabeki wa timu pinzani kwenye wingi ya kulia, kabla ya kupiga krosi ya nyuma, ambayo alipaisha mpira huu akiwa kwenye nafasi nzuri.

Fabrice Ngona naye aliunganisha vibaya faulo ya Ahoa, dakika moja kabla ya mapumziko, mpira pia ukapaa juu ya lango.

Kipindi cha pili Simba ilizidisha mashambulizi na kufanikiwa kupata bao la kwanza lililowekwa wavuni na Kibu

INAENDELEA UKURASA 23



Beki wa Simba, Shomari Kapombe, akiokoa hatari kwa kichwa dhidi ya mchezaji wa CS Constantine ya Algeria kwenye mechi ya Kundi A Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 2-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Ramovic: Ushindi kirahisi Ligi Kuu Bara umetuponza CAF

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Saed Ramovic, amesema moja ya sababu zilizofanya timu yake ishindwe kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni udhaifu wa Ligi ya Tanzania, ambayo haina timu nyingi ngumu na zenye ubora, nguvu na kasi, ambazo zingesababisha timu yake kuzoea hali hiyo.

Akizungumza juzi baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger ya Algeria, wakilazimishwa suluhu Uwanja wa Benjamin Mkapa, na kushindwa kufuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi A, Ramovic, aliwasifu wachezaji wake kwa kupambana kadri ya uwezo wao, lakini walikutana na timu ngumu, yenye wachezaji bora na wazoefu, tofauti na wale ambao wanakutana nao kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Tunapaswa kuwa wakweli kwamba ligi ya hapa Tanzania, ugumu unaokutana nao unapocheza dhidi ya timu nyingine za Tanzania si wa kiwango kikubwa sana. Ukiona ligi za Algeria, Afrika Kusini, Morocco, Tunisia, tunahitaji nguvu hiyo ya juu ili kushindana na tuweze kuzoea hali hiyo.

"Ukali wa ligi ya Tanzania, ni mdogo sana ukilinganisha na nchi hizo, wao ligi yao ni ngumu na kila timu kali sana, tunahitaji ugumu kama wa ligi hizo ili tushindane," alisema kocha huyo.

Alisema urahisi wa kupata ushindi katika michezo ya Ligi Kuu hauwajengi, badala yake unawafanya kudumaa na kupata shida wanapocheza na timu ambazo zinatoka kwenye ligi zenye ushindani, akisema suala hili likifanyiwa kazi haitokuwa faida kwa Yanga tu, bali kwa timu zote nchini ambazo zitakwenda kucheza mechi za kimataifa.

Aliwasifia wapinzani wao, MC Alger ambao walicheza zaidi nyuma ya mpira na kuwapa kazi kubwa kufungua kutokana na kuwa bora kwenye sanaa ya uzuiaji.

"Haikuwa rahisi kuweza kuwafungua, walicheza nyuma ya mpira, tulijitahidi sana, lakini sanaa yao ya uzuiaji ilikuwa nzuri na bora," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alikiri kuwa wapinzani wao walichanga karata yao

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >